SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mume** amsamehe mke aliyemjeruhi kwa chuma kizito UKURASA 3



**KLOPP: LIVER IPO TAYARI KWA UBINGWA** UKURASA 22

Nipashe
Jumatatu Machi 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580884
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Wastaafu 51,000 walipwa mabilioni

• **Ni** agizo la Rais Samia, maelfu walamba pensheni za kila mwezi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
### KAMATI KUCHUNGUZA VIFO SAMAKI MTO MARA
SERIKALI imeunda kamati ya kitaifa kuchunguza uchafuzi wa mazingira kwenye Mto Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea ndani ya mto huo mwanzoni...

UKURASA WA 15
### WALIA KUKOSA ENEO KUZIKANA
KATA ya Msalato jijini Dodoma inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa huduma za kijamii ikiwamo eneo la makaburi...

UKURASA WA 18
### VIGOGO TAMISEMI WASHUSHWA VYEO
WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amemwelekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI...

## Watanzania waliokimbia vita Ukraine wafika Poland
UKURASA 3



Sehemu ya kiwanda cha kutengeneza magodoro cha GSM kilichoteketea kwa moto Mikocheni mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JENIFER GILLA**



Mwenyekiti wa GSM Group Ltd, Ghalib Mohamed

## GSM yafunguka kiwanda kuungua
UKURASA 3

**MICHEZO** **AUCHO, USHINDI WAMTULIZA NABI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Sinyamule (wapili kushoto), akimpongeza mshindi wa promosheni ya Vodacom Tusua Mapene, Justine Kinyamonga (katikati), mkazi wa Shilabela mjini Geita, baada ya kukabidhiwa gari aina ya Suzuki S Presso aliyojishindia kupitia promosheni hiyo. Kushoto ni Meneja Mauzo Mwandamzi, Ahmed Akbarali na familia ya Kinyamonga. Hafla hiyo ilifanyika kwenye viwanja vya Shilabela, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MWAKA MMOJA SAMIA IKULU

# Tril. 1.5/- zatolewa mafao ya wastaafu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umelipa mafao yenye thamani ya Sh. trilioni 1.15 kwa wanufaika, yaani wastaafu na wategemezi 51,079.

Vilevile, mfuko umelipa Sh. bilioni 692.38 za pensheni ya kila mwezi, sawa na wastani wa Sh. bilioni 57.7 kila mwezi kwa wastaafu 147,459.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo jana alipotoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hii ni katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais yaliyotolewa katika sherehe za Mei Mosi, 2021, ambapo alielekeza madai ya mafao ya wastaafu yaliyocheleweshwa yaanze kulipwa kuanzia mwezi Mei, 2021 na kuendelea kulipwa hadi mrundikano utakapokwisha.

"Kiasi hiki cha fedha hulipwa kila ifikapo tarehe 25 ya mwezi husika bila kukosa. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, mfuko umekamilisha kulipa madai yote ya muda mrefu," alisema.

Prof. Ndalichako alisema kuwa katika kuongeza kasi ya ulipaji mafao kwa wastaafu, serikali pia imelipa jumla ya Sh. trilioni 2.17 kupitia hati fungani.

"Fedha hiyo ni sehemu ya deni la Sh. trilioni 4.6 iliyotumika kufanya malipo kwa wanachama waliostaafu ambao hawakuchangia katika kipindi cha kabla ya mwaka 1999," alifafanua.

Waziri huyo pia alisema katika kipindi hicho, serikali imelipa Sh. bilioni 200 kati ya deni la Sh. bilioni 431 la mikopo ya uwekezaji lililokuwapo wakati serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani.

Vilevile, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja, PSSSF imesajili wanachama wapya wapatao 21,461, sawa na asilimia 116.74 ya lengo la kusajili wanachama wapya 18,384 kwa kipindi husika.

"Wanachama hawa waliondikishwa kwa zaidi ya asilimia 60 wametokana na ajira mpya za kada za afya na walimu walioajiriwa na serikali katika awamu ya sita," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa katika kuhakikisha wafanyakazi wanapata maslahi na haki zao za mafao, NSSF pia imeongeza kasi ya kusajili wanachama.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita, mfuko umeandikisha jumla ya wanachama wapya 185,288, sawa na ongezeko la asilimia 19 kulinganishwa na wanachama wapya 155,192 walioandikishwa katika kipindi cha mwaka mmoja ulioishia Februari, 2021," alisema.

Alibainisha kuwa kati ya wanachama hao, wanachama 153,119 waliandikishwa kutoka sekta rasmi na wanachama 32,169 waliandikishwa kutoka sekta isiyo rasmi.

Mfuko pia uliandikisha waajiri wapya 1,605, hivyo kufanya idadi ya waajiri kufikia 34,049 sawa na ongezeko la asilimia 4.9, kwa mujibu wa waziri huyo.

Alisema katika kipindi hicho, mfuko umekusanya michango ya Sh. bilioni 1,129.4 sawa na ongezeko la asilimia tano ya michango ya Sh. bilioni 1,075.3 iliyokusanya katika kipindi cha mwaka mmoja ulioishia Februari 2021.

"Aidha, mfuko umefanya mapitio ya Mpango wa Uchangiaji wa Hiari ili kuvutia wanachama wapya kutoka katika makundi mbalimbali ikiwamo vijana waendesha bodaboda na bajaji, kinamama, wanavyuo, wakulima na wavuvi.

"Ili kuongeza wigo wa wanachama na mafao yanayokidhi mahitaji ya makundi hayo, mpango wa uchangiaji wa hiari umeboreshwa na utazinduliwa rasmi hivi karibuni," alisema Prof. Ndalichako.

Aliongeza kuwa katika kuboresha mafao ya fidia kwa wafanyakazi, serikali imeongeza kiwango cha juu cha pensheni kutoka Sh. 3,685,852.69 na kufikia Sh. 8,400,000.00 kwa mwezi.

"Ongezeko hili limekuwa faraja kubwa kwa wafanyakazi na waajiri nchini na linachangia kupunguza umaskini kwa wategemezi wa wafanyakazi wanaofariki dunia kutokana na kazi," alisema.

## SAMAKI KUFA MTO MARA

# Kamati ya kitaifa kuchunguza kiini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeunda kamati ya kitaifa kuchunguza uchafuzi wa mazingira kwenye Mto Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea ndani ya mto huo mwanzoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi jioni kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Lulu Mussa, kamati hiyo itakuwa na wajumbe 11.

Lulu alisema kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameunda kamati hiyo ya kitaifa ili kuchunguza uchafuzi wa mazingira uliojitokeza hivi karibuni ndani ya Mto Mara baada ya kutembelea eneo hilo.

Alibainisha kuwa kamati hiyo inaongozwa na Mwenyekiti Prof. Samwel Manyele, kutoka Idara ya Uhandisi wa Kemikali na Madini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Aliwataja wajumbe wengine kuwa ni: Dk. Samuel Mafwenga - Mkurugenzi Mkuu Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambaye ni katibu wa kamati; Dk. Kessy Kilulya - Mkuu wa Idara ya Kemia UDSM; Dk. Charles Kasanzu kutoka Idara ya Jiolojia UDSM; Daniel Ndio, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Wengine ni Renatus Shinhu, Mkurugenzi wa Bonde Mamlaka ya Bonde la Maji la Ziwa Victoria; Baraka Sekadende, Mkurugenzi wa Kituo - Taasisi ya Utafiti wa Samaki (TAFIRI) Mwanza; Dk. Neduvoto Mollel kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Usimamizi wa Viatilifu (TPHPA); Asnath Kauya kutoka Ofisi ya Rais; Yusuph Kuwaya Kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara; na Faraja Ngerageza - Mkurugenzi Msaidizi - Ofisi ya Makamu wa Rais.

Lulu alisema kuwa kamati hiyo imetakiwa kutoa taarifa ya uchunguzi ndani ya siku saba kuanzia juzi na kuiwasilisha kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ifikapo Machi 19, 2022.

Juzi Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria ilitoa matokeo ya uchunguzi wa sampuli za maji waliyopima katika maabara yao kuhusu tukio hilo.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha samaki hao wamekufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni kutokana na kuwapo mafuta aina ya oili na grisi yaliyotanda juu ya maji eneo la Mto Kirumi.

Mwanzoni mwa mwezi huu, samaki walionekana wakielea huku wakiwa wamekufa katika mto huo na kuzua taharuki kwa watu wanaopakana na eneo hilo.

## HABARI KITAIFA

# Watanzania waliokimbia Ukraine wafika Poland

**Na Salome Kitomari**

WANAFUNZI 32 waliotoka Chuo cha Sumy, Ukraine wamefanikiwa kufika Poland na Hungary, huku wakimshukuru Balozi wa Tanzania Ujerumani, Dk. Abdallah Possi, kuwapokea baada ya kuwasili.

Mwanafunzi wa kiume (jina tunalihifadhi), aliiambia Nipashe jana kuwa baadhi ya wenzao wengine, walifika salama Poland, huku wengine wakiamua kubaki kwenye nchi hizo kutafuta namna ya kuendelea na vyuo, kupumzika na baadhi wakiamua kurudi nyumbani.

Wanafunzi hao walianza safari Machi 10, mwaka huu, wakitokea chuoni Sumy mjini Poltavo kuelekea mpaka wa Hungary na Poland ili kukimbia vita vinavyoendelea Ukraine.

Kijana huyo alipozungumza na Nipashe Machi 12, mwaka huu, wakiwa Mji wa Kiev, alibainisha kuwa walifanikiwa kufika mpakani Lviv.

"Tumetoka Lviv hadi Chop tumefika saa nne usiku kwa kuwa mpaka uko Chop, tulikaa kwa muda mrefu na kufanikiwa kuvuka saa 11:30 asubuhi (Machi 12), tumechoka sana na bado tunatakiwa kuendelea na safari kwenda Budapest mjini Mkuu wa Hungary, tumepambana wenyewe sana haikuwa rahisi ila ilibidi tukubaliane na mazingira. "Nimefanikiwa kufika salama Hungary na wengine wamefika Poland, mimi ni mzima wa afya na wenzangu pia, Mungu anazidi kututetea, tulitoka mpakani mwa Hungary na Ukraine na kupanda treni hadi Budapest ambako ni Mji Mkuu wa Hungary.

"Tulipokewa na Watanzania wenzetu, tukakutana na Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, aliongea na sisi. Baadaye kila mtu akabaki na mipango yake.

"Kuna walioamua kurudi Tanzania na wengine wamebaki kama mimi, wengine wanataka kutafuta vyuo waendelee na masomo, wengine wafanye kazi huku wakisubiri taarifa kutoka chuoni kama masomo yataendelea kwa njia ya mtandao au tutarudi tena chuoni baada ya vita kuisha," alisema.

Mwanafunzi huyo alisema gharama za maisha kwenye nchi hiyo wanajilipia kwa kusaidiwa na wazazi wao wanaowatumia fedha.

"Nimeamua kubaki hapa ila tumetafuta nyumba ya bei rahisi ili nisimuumize mzazi wangu, wanatupa fedha ya kodi, chakula na mahitaji mengi. Mimi nina sababu za msingi kama kupata chuo cha kuendelea na masomo, wapo wengine wanajaribu kutuliza akili kutokana na magumu waliyopitia wakiwa Ukraine," alisema.

Alibainisha kuwa wote wamepewa visa ya siku 47 kutembea nchi zote za Umoja wa Ulaya na wanaruhusiwa kuhuisha, na kwamba walipofika mpakani walipewa visa kwa sababu wanajulikana wametokea Ukraine ambako kuna vita kwa sasa.

# Mume amsamehe mke aliyemjeruhi

**Na Said Hamdani,** LINDI

ZAINABU Mahamoka (35), mkulima wa Kijiji cha Makonjiganga, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, amenusurika kufikishwa mahakamani kwa kosa la kumjeruhi kwa kumpiga na kitu kizito mumewe, Hemedi Nyanyweleka na kumsababishia majeraha.

Nyanyweleka na Zainabu ni wanandoa na wana mtoto mmoja wa kike wa miezi mitatu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kijijini huko zilizothibitishwa na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mariamu Malua, tukio hilo lilitokea Machi 4, mwaka huu, majira ya mchana, chanzo kikidaiwa kuwa ni ulevi wa mume.

Malua akizungumza na mwandishi wa habari hizi, alisema baada ya kugombana mumewe akiwa amelewa, mkewe alichukua chuma na kumpiga kichwani mumewe aliyeanguka chini na kupoteza fahamu.

Alisema kuwa mumewe alipelekwa Kituo cha Polisi akapatiwa PF3 na kukimbizwa Hospitali ya Wilaya Liwale kwa ajili ya matibabu na mkewe alikamatwa na kupelekwa polisi, lakini mume alipozinduka alijulishwa kuwa mkewe ndiye kamjeruhi.

"Mume alipozinduka na kuelezwa mzazi mwenzake anahitajika kupelekwa mahakamani kujibu shtaka la kujeruhi, akaomba asipelekwe kwa kuwa ana mtoto mchanga," alisema Malua.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya, alipoulizwa juu ya tukio hilo, alisema hana taarifa huku akidai hata kama lingemfikia, kwa vile mlalamikaji alishamsamehe mtuhumiwa, polisi hawana uamuzi zaidi.

# GSM yafunguka kiwanda kuungua

**Na Jenifer Gilla**

KIWANDA cha kutengeneza magodoro kinachomilikiwa na Kampuni ya GSM kilichoko Mikocheni mkoani Dar es Salaam, kimeungua moto, huku chanzo cha moto huo kikiwa bado hakijajulikana.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa wasimamizi wa kampuni hiyo, Salah Mohamed, alisema alipata taarifa za kuungua kwa kiwanda hicho majira ya saa 12 asubuhi.

"Nilipigiwa simu majira ya saa 12 asubuhi na kaka yangu akiniambia kuwa 'bwana GSM foam Mwenge pale panawaka moto, hebu angalia nini tunaweza kufanya'.

"Kwa hiyo, nikafika haraka na tukaanza kufanya mawasiliano. Ninalishukuru Jeshi la Polisi walifika mapema tu," Salah alipongeza.

Alisema kuwa baada ya kufanya mawasiliano sehemu mbalimbali, walifanikiwa kupata magari ya zimamoto na kuzima moto huo, lakini mali kwenye ghala hilo zilikuwa zimeshateketea.

"Kwa kweli mpaka sasa hatujui ni kiasi gani cha mali kimeteketea, ninachoweza kusema hasara ni kubwa sana. Kama unavyoona, hakuna kilichosalia," alifafanua.

Alisema thamani halisi ya mali zilizoteketea itajulikana baada ya kufanyika kwa tathmini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Zimamoto Kinondoni, Christina Sungwa, alisema walipokea taarifa ya tukio hilo asubuhi.

"Baada ya kupata taarifa ya tukio la moto, tulifika haraka eneo la tukio, tukaomba msaada kwa wenzetu wa bandari na kampuni binafsi wanaohusika na shughuli za uzimaji moto," alisema.

Nipashe ilishuhudia magari ya zimamoto yakiendelea na uzimaji wa moto katika eneo hilo, huku majengo ya ghala hiyo yakiwa yameteketea kwa moto.

Wafanyakazi pamoja na wamiliki wa kiwanda hicho wakiwa kwenye majonzi, walikusanyika kuangalia mabaki ya mali zilizoteketea kwa moto.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema moto ulioteketeza kiwanda hicho ulidhibitiwa usilete madhara nje ya eneo hilo.

"Nampongeza kamanda mwenzangu wa zimamoto pamoja na vikosi vingine vilivyoshiriki, kazi imekwenda vizuri wamejitahidi hatujapata madhara mengine zaidi ya eneo hili," alisifu Kamanda Muliro.

**"Nilipigiwa simu majira ya saa 12 asubuhi na kaka yangu akiniambia kuwa 'bwana GSM foam Mwenge pale panawaka moto, hebu angalia nini tunaweza kufanya'.**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASAJILE MACLEAN MWAKANOSYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 256 BXE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/TUK/RB/579187/2022**

## NYUMBA INAPANGISHWA

**MAHALI:** KIHARAKA MAPINGA KARIBU NA KANISA LA TAG NI NYUMBA MPYA YA VYUMBA 3, SEBULE, JIKO NA PUBLIC TOILET KWA MAWASILIANO PIGA SIMU: **0655-529509 / 0711-622282 / 0714-421555**

IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2022

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DR. BATIMO DONALD SEBYIGA DECEASED OF NKUHUNGU-DODOMA

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PATRICK BATIMO SEBYIGA

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of the Probate Rules GN NO. 369 OF 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 18/03/2022.

Dated at Dodoma this 10 day of 03/ 2022.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT




## KUKARIBISHA MAWAKALA WA KUSAMBAZA GESI KUTOKA KAMPUNI YA PUMA

Puma Energy Tanzania ni kampuni ya mafuta iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huku ikiwa inamilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri wa Muungano (kupitia Msajili wa Hazina) pamoja na Puma Investments Limited kwa hisa za asilimia 50 kwa kila moja. Kampuni ya Puma ni kampuni ya kimataifa ya kuuza mafuta inayojishughulisha na uhifadhi na usambazaji mkubwa wa bidhaa za diesel na petrol.

Kampuni hii ndio inaongoza kwenye soko kwa hapa Tanzania kwa kumiliki soko huku ikiwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta kiasi cha lita milioni 94, ikiendesha vituo vya mafuta 69 nchini pamoja na kutoa huduma ya mafuta ya ndege katika viwanja vya ndege vinane 8 kote hapa nchini.

Puma Energy Tanzania imekusudia kuingia sokoni kuuza na kusambaza gesi ya kupikia majumbani, au kitaalamu Liquefied Petroleum Gas (LPG). Bidhaa hii itapatikana katika ujazo wa kilo 6, kilo 15 na kilo 38. Tunakaribisha maombi kwa wanaotarajia kuwa wasambazaji wakubwa wa PumaGas nchini kote ambao watakuwa wanasambaza gezi kwa jumla na reja reja. Mawakala hao wanaweza kuwa mtu binafsi, ushirikiano au kampuni.

Mawakala hao wanatakiwa kuthibitisha vigezo vifuatavyo:

1. **Leseni ya biashara**
2. **Cheti cha ukaguzi kutoka kwa Jeshi la Zima Moto kwa duka au ghala**
3. **Mizani ya kupimia iliyokaguliwa**
4. **Uwepo na kituo salama cha uhifadhi au ghala**
5. **Uwezo wa kuaminika wa kusambaza – Ufikishaji bidhaa kwa walaji**

Mwisho wa kutuma maombi ni 31 Machi 2022. Maombi yote yanatikwa kutumwa kwa novatus.mdee@pumaenergy.com. Puma Energy Tanzania itawasiliana na wale ambao wataokuwa wametimiza vigezo.

Waombaji wanaweza kupata taarifa zaidi kwa kutembelea tovuti yetu www.pumaenergy.com au wanaweza kutembelea ofisi zetu ambazo zipo barabara ya Bandari, Kurasini, Dar es Salaam.

ISO 9001-2015 AND ISO 14001 – 2015 CERTIFIED
Kurasini Bandari Road
P.O. Box 9043, Dar es Salaam, Tanzania
Switchboard: (22) 2111269-272
Central Fax: (22) 2112726/7, 2112724
www.pumaenergy.com

216740702



TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

# Mafanikio ya sekta ya Ushirika katika mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita

## Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 yenye majukumu ya kudhibiti na kusimamia Vyama vya Ushirika pamoja na uhamasishaji wa maendeleo ya sekta ushirika nchini ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ambayo ipo chini ya Wizara ya Kilimo.



*Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan*

## Majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Majukumu makuu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni pamoja na: Kuandikisha na kufuta vyama vya ushirika; Kukagua na Kusimamia vyama vya ushirika; Kutunza na kuboresha rejista ya vyama vya ushirika; Kutatua migogoro na malalamiko katika vyama vya ushirika; Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo endelevu na ya kiuchumi ya vyama vya ushirika; Kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama na watumishi wa vyama vya ushirika kuhusu uendeshaji wa ushirika; Kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa za vyama vya ushirika; na Kufanya tafiti mbalimbali kwa maendeleo ya vyama vya ushirika.



*Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe (kulia) akiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Anthony Mavunde*

## MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege (kushoto) na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga*

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika, ambapo jumla ya Vyama vya Ushirika 6,013 kati ya Vyama 9,185 vilikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo ni pamoja na kubaini kuwepo ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji katika baadhi yaVyama vya Ushirika, na hivyo kusababisha kutokea kwa vitendo vya wizi na ubadhirifu wa fedha na mali za Vyama hivyo. Aidha, ilibainika kuwa baadhi ya vyama vya ushirika vina mifumo mibovu ya udhibiti wa ndani na vinashindwa kuandika miamala ya fedha kulingana na taratibu za fedha zilizopo. Hatua zilizohukuliwa ni pamoja na kuwaondoa/kuwatengua Viongozi wa Bodi za Vyama na watendaji waliobainishwa kuhusika na vitendo vya wizi na ubadhirifu na kufikishwa kwenye vyombo vya Dola kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria.

Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanza utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo wa kuwajengea uwezo Maafisa Ushirika nchini katika eneo la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 Maafisa Ushirika 170 kutoka mikoa 13 walikwishanufaika na mafunzo hayo. Hatua nyingine iliyochukuliwa na Tume ni kununua vitendea kazi ambapo magari 15, pikipiki 137 na kompyuta 82 zimenunuliwa. Tume pia ipo katika hatua za mwisho za uundaji Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2022.



*Baadhi ya pikipiki na magari yaliyonunuliwa na Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kabla ya kukabidhiwa kwa Wasimamizi wa Vyama vya Ushirika, Mikoani na Wilayani*

## Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

Katika eneo la usimamizi wa vyama vya ushirika, Tume imesimamia Chaguzi za viongozi katika Vyama vya Ushirika 420 ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa na wanachaguliwa viongozi wenye sifa. Aidha, Tume imeendelea pia kuchakata maombi ya Leseni za uendeshaji wa SACCOS ambapo SACCOS 172 zilipatiwa Leseni na hivyo kufanya idadi ya SACCOS kufikia 615. Kati ya hizo, SACCOS Daraja A ni 486 na SACCOS Daraja B ni 129, ambapo jumla ya maombi 267 yalirudishwa kwa ajili ya kufanya maboresho katika nyaraka zilizowasilisha.





## TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

# Mafanikio ya sekta ya Ushirika katika mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita

**Udhibiti wa Migogoro**

Serikali kupitia Tume imeendelea kudhibiti migogoro katika Vyama vya Ushirika ambapo jumla ya migogoro 68 ilitatuliwa. Ili kudhibiti kutokea kwa migogoro mipya, Tume imeendelea kutoa elimu ya Ushirika kwa viongozi wa vyama na wanachama kupitia mikutano mikuu ya Vyama vya Ushirika na Vyombo vya Habari.

**Uhamasishaji wa Uanzishwaji wa Vyama**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kufanya uhamasishaji wa uanzishwaji wa vyama vya ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Katika mwaka 2021/2022, Tume imeratibu na kushiriki Uhamasishaji wa uanzishwaji wa Chama cha Ushirika cha wataalamu wa ukuzaji viumbe maji waliopo katika sekta ya Uvuvi kote nchini. Jumla ya washiriki 250 wamefikiwa na kupatiwa elimu juu ya taratibu za kuanzisha Chama kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo mingineyo ya Ushirika. Aidha, Tume imefanya uhamasishaji kwa vikundi 54 vyenye jumla ya wakulima 1,440 katika Halmashauri ya Muheza na Korogwe mkoani Tanga, Halmashauri ya Siha na Mwanga mkoani Kilimanjaro na Halmshauri ya Arusha na Ngorongoro mkoani Arusha. Vilevile, jumla ya wanakikundi 800 ambao ni wafugaji ndani ya Tarafa ya Ngorongoro wamepatiwa mafunzo bora kuhusu ufugaji Nyuki ambapo Mizinga 1,476 ilitolewa kwa vikundi vyote na taratibu za kuvisajiri vikundi hivi kuwa Vyama vya Ushirika unaendelea.

Hatua hizi zote zimewezesha kusajiliwa kwa Vyama vya Ushirika 40 na hivyo kufanya idadi ya vyama kufikia 9,741 na kuongezeka kwa idadi ya wanachama wa vyama vya Ushirika hadi kufikia 6,965,272,672 mnamo mwezi Disemba, 2021.

**Kuimarisha Huduma za Ugani**

Kuhusiana na kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima na kuongeza tija kwenye kilimo, Tume imehamasisha Vyama vya Ushirika kuanza kuajiri Maafisa Ugani ili kuongeza tija. Hadi Juni, 2021 kuna Jumla ya Maafisa Ugani 76 waliajiriwa na Vyama vikuu vya Ushirika vitano (KCU Ltd, KDCU Ltd, KACU Ltd, MAMCU Ltd, TANECU Ltd, KNCU Ltd)

**Upatikanaji wa Pembejeo Kupitia Ushirika**

Vyama vya ushirika vimefanikisha upatikanaji wa pembejeo kupitia mfumo wa ushirika ambapo katika mwaka 2020/21 mbolea tani 22,175 zenye thamani ya Shilingi 6,018,386,364, mbegu na viuatilifu tani 252 vyenye thamani ya Shilingi 860,645,250, mbolea tani 17,237.44 zenye thamani ya Dola za Marekani 11,756,830.51, na madawa na vifungashio vyenye thamani ya Dola za Marekani 820,054.34 vilinunuliwa. Katika miaka ya nyuma utaratibu kama huo haukuwepo na wakulima walinunua kutoka kwa wanunuzi binafsi ambao waliwauzia kwa bei kubwa na ubora mdogo. Pembejeo zote za pamba na tumbaku kwa mwaka 2020/21 zimeagizwa na ushirika.



*Ghala la Pembejeo za Korosho zilizonunuliwa kupitia Ushirika mkoani Mtwara*

**Masoko ya Mazao ya Wakulima na Wanaushirika**

Vyama vya ushirika vinaratibu masoko ya mazao ya wakulima na wanaushirika kwa mazao ya kimkakati na mengine. Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabaddhi za Ghala na Soko la Bidhaa kwa pamoja wamehamasisha na kutoa elimu kwa vyama vya ushirika kuhusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwenye zao la choroko, dengu, Kakao na ufuta katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Katavi, Songwe,

Rukwa, Mbeya, Singida, Dodoma, Geita, Morogoro na Iringa.



*Mnada wa Korosho mkoani Mtwara*

Mfumo huu umelenga kuwakomboa wakulima kwa kuwahakikishia upatikanaji wa soko na bei nzuri. Mfumo huu umewawezesha wakulima kupata bei bora ya mazao yao. Kwa mfano, bei ya korosho ilipanda kutoka shilingi 1,300 hadi 3,000 kwa kilo. Kakao kilo moja iliuzwa kati ya shilingi 1,800 hadi 2,500 kabla ya mfumo na baada ya kuanzisha mfumo wa stakabadhi kilo moja imeuzwa hadi shilingi 4,800 mpaka 5,000. Pia, awali zao la Ufuta kilo moja iliuzwa shilingi 1,000 mpaka 1,500 na baada ya kuanzisha mfumo wa stakabadhi kilo moja imeuzwa zaidi ya shilingi 2,500 mpaka 3,500.

| Na. | Zao | Kiasi (Kgs) | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | Pamba | 122,789,149 | 165,765,351,150 |
| 2 | Korosho | 231,102,919 | 488,986,356,596 |
| 3 | Mkonge | 4,934,831.80 | 18,784,149,883 |
| 4 | Kakao | 4,592,782 | 22,929,163,568 |
| 5 | Ufuta | 81,447,042 | 195,355,744,626 |
| 6 | Mbaazi | 3,013,538 | 3,938,150,669 |
| 7 | Soya | 1,090,199 | 1,611,939,457 |
| 8 | Kahawa | 59,278,154 | 410,522,544,767 |
| 9 | Tumbaku | 57,367,188.49 | 204,420,711,000 |
| 10 | Chai | 9,679,934 | 3,097,578,880 |
| | **Jumla** | **575,295,737.29** | **1,515,411,690,596** |

*Mazao ya kilimo yaliyouzwa kupitia ushirika kuanzia July 2021 mpaka Februari 2022*

Pia, Tume inashirikiana na NFRA na Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili kununua mazao ya wakulima kupitia ushirika na kuongeza wigo wa masoko ya mazao ya wakulima. Vyama vya ushirika vinauza pia mazao ya wakulima moja kwa moja kwenye masoko ya nje (direct sell). Tume ya maendeleo ya ushirilka imeendelea kuwajengea uwezo wa kibiashara na masoko watendaji na viongozi wakuu wa vyama vikuu vya ushirika kwa kufanya mafunzo ya biashara na masoko kwa mwaka mara mbili.



*Washiriki wa Mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kibiashara na Masoko Watendaji na Viongozi wakuu wa Vyama Vikuu vya Ushirika*

Aidha, Tume imefanya ziara ya mafunzo, tafiti na masoko ya kahawa kwa kushirikisha Chama Kikuu cha Kagera (KCU Ltd) kwa lengo la kuendelea kuongeza wigo wa kutafuta masoko ya mazao ya wanaushirika.

**Kuimarisha Elimu ya Ushirika**

Elimu ya Ushirika inazidi kuimarika miongoni mwa wananchi. Tume inatumia vyombo vya habari kama televisheni kutoa elimu ya ushirika kwa wananchi. Katika eneo hili, Tume imeshirikiana na Vyombo vya Habari (Televisheni, Redio na Magazeti) kutoa Makala mbalimbali za Ushirika; ikiwemo kuanzisha Kipindi cha Kila Wiki katika Televisheni na Redio ya Taifa (TBC1 na TBC Taifa). Pia imeimarisha matumizi ya mitandao ya kijamii katika kuhabarisha umma juu ya manufaa ya Ushirika.



*Wanaushirika Mkoani Arusha wakiwa katika Mafunzo ya Elimu ya Ushirika*

**Viwanda Vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika**

Kupitia uhamasishaji, viwanda vidogovidogo na vikubwa vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vimeongezeka ambapo hadi kufikia Februari 2022 Vyama vya Ushirika vilianzishwa na kufufuliwa na kufanya jumla ya viwanda kuwa 452 ikilinganishwa na viwanda 374 mwaka 2019/20. Kati ya hivyo vipo viwanda vya kuchambua pamba vya KACU na CHATO vilivyofufuliwa msimu wa 2019/2020 na kiwanda cha kuchambua Pamba cha MBOGWE 2020/2021 kimefufuliwa na sasa kinachachakata pamba za wanaushirika. Viwanda vingine ni vya mazao ya kahawa, Mkonge na Alizeti.



*Chama Kikuu cha Songea na Namtumbo (SONAMCU) kinajenga Kiwanda cha Vifungashio*

**Ajira na Upatikanaji wa Huduma za Kijamii katika Vyama**

Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika kumefanikisha kuongeza ajira kwa wananchi kupitia Ushirika kufikia ajira 100,100 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na ajira 90,090 kwa mwaka 2019/20.

Aidha, Vyama vya Ushirika vimekuwa chachu ya wananchi kupata huduma za kijamii. Mfano, vyama vya Ushirika vimeanza kutoa huduma ya Bima ya Afya kwa wanachama wake kwa kushirikiana na NHIF na mabenki. Mkakati umewekwa kati ya Tume na NHIF kuhakikisha wanachama wa vyama vya ushirika wanapata huduma ya afya ya uhakika kwa wakati. Wakulima zaidi ya milioni moja wameishajiunga kwenye mpango huu.



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dkt. Benson Ndiege, (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga wakionesha Mkataba wa Makubaliano ambapo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unawawezesha wakulima walioko ndani ya Vyama vya Ushirika nchini kujiunga na huduma za matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya unaojulikana kama Ushirika Afya.*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zipambane kuifikia Simba si kuirudisha zilipo

**JANA** wawakilishi pekee wa michuano ya kimataifa nchini, Simba, walishuka Uwanja wa Benjamini Mkapa kuikaribisha RS Berkane ya Morocco kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mechi hiyo ilikuwa ya marudiano baada ya ile ya awali wiki mbili zilizopita nchini Morocco, Simba kukubali kichapo cha mabao 2-0, hivyo kumaliza mzunguko wa kwanza ikiwa na pointi nne sawa na USGN ya Niger huku RS Berkane ikivuna alama sita kileleni na Asec Mimosas ikiburuza mkia kwa pointi zake tatu.

Hivyo, matokeo ya jana kwa timu hizo nne yalitarajiwa kubadili msimamo mzima wa kundi hilo ambalo linaelezwa kuwa gumu zaidi kuliko makundi mengine kwenye michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Kwa ujumla kila mwenye nia njema ya kuona soka la Tanzania linapiga hatua na nchi kutangazika kimataifa kimichezo, hana budi kuendelea kuitakia mema Simba kusonga mbele katika michuano hii.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba, hakuna njia ya mkato kwa Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu msimu ujao; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, kama Simba hatafanikiwa kufuzu robo fainali na kuendelea mbele zaidi.

Ikumbukwe hadi sasa imebaki nafasi moja tu kwa nchi ambazo zinawania kuwa miongoni mwa mataifa 12 yatakayopata tiketi ya kuingiza timu 12 katika michuano hiyo msimu ujao, hivyo njia pekee ya kwa Tanzania kukata tiketi hiyo ni Simba kufika mbali katika michuano hii.

Lakini mbali na Tanzania inayowania nafasi hiyo kwa karibu, kuna Libya ambayo ina timu mbili zinazoiwakilisha kwenye michuano hiyo, hivyo ina nafasi kubwa ya kukata tiketi hiyo, endapo tu Simba haitatinga robo fainali na timu zao kufika hatua hiyo na zaidi.

Hata hivyo, wakati tulitarajia kuona wadau wa soka nchini na, mashabiki na Watanzania kwa ujumla wakiungana kuwa kitu kimoja katika kuisapoti Simba ili kupigania nafasi hizo nne, wapo baadhi ambao wanajifanya kujitoa ufahamu kwa kutoona umuhimu huo na wanachotaka ni kuwashusha wawakilishi wetu hao kimataifa ili warejee walipo wao.

Ndiyo, tunasema hivyo hasa baada ya kushuhudia baadhi ya mashabiki wapinzani wa ndani wa Klabu ya Simba jana wakiishangilia RS Berkane kama ilivyokuwa Ijumaa iliyopita walipojitokeza kwa wingi kwenda kuipokea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere huku wakieleza dhamira yao ya kuwaona wawakikilishi wa Tanzania wakiishia hatua hiyo ya makundi.

Si hilo tu, lakini wapo baadhi tena viongozi wakuaminika katika mchezo uliopita ambao Simba ilishinda mabao 3-1 dhidi ya Asec Mimosas katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, walithubutu kutoa kauli za kipuuzi eti wakiwataka wapinzani hao wa Simba kuwa makini katika vyumba vya kubadilishia kutokunywa maji ya wenyeji wao uwanjani.

Sisi tunasema huu ni ushabiki uchwara na ulimbukeni uliopitiliza kwani kwa kauli kama hizo huzichafui Simba pekee bali Tanzania kwa ujumla, hivyo hatuna budi kila mmoja kwa nafasi yake kuzikemea kwa nguvu zote huku tukiimiza umoja na mshikamano katika kuwasapoti wawakilishi wetu wa nchi kimataifa.

Tanzania ni nchi ya amani na salama kwa wageni na wenyeji, lakini tunaamini Klabu ya Simba ina viongozi weledi na makini ambao wamewahi kushika nyadhifa kubwa serikalini, hivyo hawawezi kushiriki kwa namna yoyote ile katika kuchafua sifa ya taifa eti kwa sababu tu ya mpira.

Hivyo, Nipashe tukiwa wadau namba moja wa soka na michezo kwa ujumla, tunapenda kuona nguvu kubwa inayotumiwa na wapinzani wa ndani wa Simba kisoka katika kutaka kuishusha hapo ilipo, ikielekezwe katika kuziinua klabu zao na zingine ili misimu ijayo tuwe na wawakilishi wengi kimataifa katika hatua hii ya makundi, robo fainali, nusu na hatimaye fainali na ikiwezekana kubeba ubingwa wa michuano hiyo miwili mikubwa Afrika.

Kwetu sisi tunaendelea kushikilia msimamo wetu wa kuziunga mkono klabu zote zinazoiwakilisha nchi kimataifa kwa kuwa yoyote ile itakayopata mafanikio ni Tanzania imeshinda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwaka mmoja wa Rais Samia kaliheshimisha soka wanawake

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ni miezi takriban saba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, pale kikosi cha Timu ya Wanawake Twiga Stars kilipotwaa Kombe la Shirikisho la Soka Ukanda wa Kusini mwa Afrika (COSAFA).

Twiga Stars ilikwenda kama mgeni mwalikwa, kwani Tanzania au Shirikisho la Soka nchini (TFF), halipo kwenye Ukanda wa COSAFA.

Kinadada wa Tanzania walifanya vema kwa kutoa vichapo kwa timu za Namibia, Botswana, Malawi, Afrika Kusini hadi ikatwaa kombe hilo. Ilikuwa ni dalili nzuri ya kuanza kung'aa kwa soka la wanawake nchini ambalo huko mwanzo lilionekana ni kama la kujifurahisha tu.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu, Somoe Ng'itu, anasema kuwa awali mpira wa miguu wa kinamama ulionekana kama ni mchezo wa kupoteza muda, na waliocheza walionekana kuwa ni wahuni waliokosa kazi, lakini kwa sasa hali imebadilika kabisa kwani wachezaji wameanza kuheshimika.

Hiyo ndiyo dhana kubwa iliyojengwa na wengi na ilisababisha wazazi na walezi wengi kuwakataza mabinti zao kucheza mchezo huo kwa kuona kuwa hautowasaidia chochote, zaidi ya kuwaharibu tu.

Mwezi huo huo wa Oktoba mwaka jana, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan aliwaita Ikulu, ambapo pamoja na kupata nao chakula, lakini kuwapongeza kwa kazi kubwa walioifanya si kwa kuleta kombe nchini, lakini kuitangaza nchi kwa ujumla.

Rais alilipokea kombe hilo, lakini naye aliagiza mabinti hao kupewa viwanja.

Machi 19, Rais Samia anatimiza mwaka mmoja tangu aingie madarakani. Lakini kwa muda mfupi tu alioingia, ameufanya mpira wa miguu kwa kinamama kuthaminiwa na kuheshimika.

Mzazi yeyote yule ambaye hapo awali alikuwa akimkataza binti yake asicheze soka kwa madai ni mchezo wa kihuni, halafu akaona tukio lile la mabinti za wenzake wakiwa Ikulu na mheshimiwa Rais, ni lazima atakuwa alijisikia vibaya.

Kama alisikia Rais akitangaza mabinti wake wapatiwe viwanja, atajuta juu ya uamuzi wake alioufanya. Na wale wote ambao walikuwa wanabezwa na wazazi wenzao kwa kuwaacha watoto wao wa kike kujitumbukiza kwenye soka, sasa wao ndiyo wanaanza kutamba.

Kwa kifupi, Rais ameliheshimisha soka la wanawake na kuonekana ni mchezo kama mingine ambayo inaweza kumfanya mtoto wa kike kupata kipato kitakachomwezesha kuishi bila kumtegemea mtu mwingine, kusaidia wazazi wake, kufahamika, lakini kufika nchi mbalimbali na maeneo ambayo hata mzazi hakuota kufika, ikiwamo Ikulu.

Nadhani kwa hali ile na ilivyo sasa mwaka mmoja tu wa uongozi wa Rais Samia, kuna wazazi wameshaanza kubadilisha mitazamo yao, kwani soka la wanawake limekuwa juu kwa sasa, na hata mashabiki wa soka la wanaume nao, wameshaanza kuanza kulifuatilia.

Tuliona mechi kati ya Simba na Yanga kwenye miezi kadhaa nyuma, ikiwa ni ya Ligi Kuu ya Wanawake jinsi mashabiki walivyojitokeza kwa wingi wakishangilia mithili ya timu za wanaume.

Na baadhi ya mechi za Ligi Kuu zimeanza kuonyeshwa laivu, zikivutia watu wengi.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wilfred Kidao, anasema kuwa kipindi kifupi tu cha Rais Samia kuwapo madarakani, Ligi Kuu ya Wanawake si tu imepanda hadhi, lakini imeanza kuwa ya kulipwa, huku wachezaji mbalimbali kutoka nje ya nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Ghana, Burundi, Nigeria, wakija nchini kujiunga na klabu mbalimbali kwa sababu imeanza kuwa na maslahi.

Ukiongea na baadhi ya wachezaji wa kike, wanakwambia kuwa tofauti na zamani, kwa sasa soka la kinamama limeanza kuwalipa, kwani wanalipwa posho na mishahara mizuri na wengine wameshaanza kuwajengea wazazi wao nyumba, pia wao wenyewe kuwawezesha kuishi kwa kazi hiyo tu ya soka, tofauti na zamani.

# Taasisi 19 za Tanzania zashiriki maonyesho Qatar

**Na Mwandishi Wetu,** QATAR

TANZANIA ni miongoni mwa nchi 130 zinazoshiriki katika Maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira yanayoendelea Doha, Qatar, ikipeleka taasisi 19.

Maonyesho hayo huwa yanafanyika kila mwaka na kwa mwaka huu yalianza kuanzia Machi 10 na yanafanyika kwa muda wa siku tano yakiwa yamejumuisha kampuni 300 za kimataifa.

Meneja Mawasiliano wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Irene John, anayehudhuria maonyesho hayo, alisema jana kuwa yalifunguliwa na Waziri wa Manispaa na Mazingira wa Qatar, Abdulla bin Abdulaziz bin Turki Al Subaiel.

Alisema lengo kuu la maonyesho hayo ni kutoa fursa kwa washiriki kuonyesha bidhaa na huduma zinazohusiana na kilimo na mazingira.

Irene alisema maonyesho hayo yanawapa fursa washiriki kubadilishana uzoefu, teknolojia pamoja kutafuta masoko na fursa na uwekezaji katika kilimo na usimamizi wa mazingira.

Alisema NEMC ni miongoni mwa taasisi 19 zinazoshiriki kutoka Tanzania na kwamba ina mabanda 19. Kati yake, 17 ni kutoka taasisi za serikali zinazoshughulika na mazingira, kilimo, ufugaji na uwekezaji.

Alizitaja baadhi ya taasisi za serikali zinazoshiriki kuwa ni pamoja na Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Qatar, NEMC, TIC, Bodi ya Korosho, Bodi ya Maziwa, Bodi ya Chai, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pamba, Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Umoja wa Kilimo cha Mboga.

Aliwataja washiriki wengine kutoka Tanzania kuwa ni MambоJambo Design, Dumas African, Greencom African Ltd, Natural Shine Traders na Kampuni ya Oasis Import Export Ltd.

Akizungumza katika maonyesho hayo, Irene alisema yatafungua fursa nyingi za uwekezaji katika bidhaa na huduma kwa kuwa kupitia mawasilisho yaliyofanywa siku ya ufunguzi, NEMC imeonyesha jinsi mazingira ya uwekezaji yameboreshwa kupitia mifumo mbalimbali ya kielektroniki.

Alisema mchakato wa utoaji vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) umerahisishwa na pia mfumo wa upatikanaji wa vibali vya taka hatarishi ambao uko katika hatua za mwisho kukamilika.

Meneja wa NEMC, Kanda ya Ziwa, Jarome Kayombo, alibainisha kuwa moja ya faida kubwa kwa NEMC kushiriki katika Maonyesho ya Kimataifa ya Mazingira na Kilimo ni pamoja na kuitangaza, pia kutoa elimu juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa uwekezaji endelevu.

Alisema maonyesho yametoa fursa za uwekezaji na kuelimisha washiriki juu ya mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira Tanzania.

# Mbaroni kwa tuhuma bangi kwenye mbaazi

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi wilayani Ruangwa mkoani Lindi linawashikilia kwa mahojiano wakulima wawili wa Kijiji cha Mibule kwa madai ya kujihusisha na kilimo cha bangi kinyume cha sheria za nchi. Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani humo, Foka Dinya, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe ofisini kwake mjini Lindi.

Alisema watuhumiwa hao aliowataja kuwa ni Awesu Mohamedi (40) na Juma Muhidini (32) wote ni wakulima wa Kijiji cha Mibule, Wilaya ya Ruangwa, walikamatwa Machi 6, mwaka huu baada ya jeshi hilo kupata taarifa kutoka kwa raia wema.

Kamanda Dinya alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, askari walifuatilia katika mashamba yanayomilikiwa na wakulima hao na kufanikiwa kukuta bangi imechanganywa na mazao mengine ya mahindi, mbaazi na ufuta.

Alisema kuwa askari wao waliharibu kwa kung'oa miche 336 ya bangi iliyokuwamo kwenye mashamba ya wamiliki hao, huku akisisitiza kwa kutoa onyo kwa wengine wanaojihusisha na kilimo cha zao hilo kwamba wataingia kwenye matatizo na mkono wa dola.

Alisema serikali iko imara na inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kulinda raia na mali zao, hivyo ni vyema walio na tabia ya kujihusisha na kilimo au biashara haramu ikiwamo ya dawa za kulevya, waiache wenyewe pasipo kusubiri mkono wa serikali.

Alisema kuwa watuhumiwa wote wawili watafikishwa mahakamani muda wowote baada ya kukamilika kwa taratibu za kiuchunguzi.

# Bonite Bottlers Ltd. yatoa ufafanuzi utapeli tangazo la kazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd imetoa ufafanuzi kuhusu tangazo la nafasi za ajira 543 linaloihusisha, ikionya kuwa haijatangaza nafasi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo, kumekuwa na tangazo linalosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba kampuni hiyo imetangaza ajira hizo kwa vijana wa Kitanzania na kwamba usaili utafanyika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro mwezi huu.

"Tunapenda kuwafahamisha kuwa taarifa hizi zinazo sambazwa mitandaoni za ajira sio za kweli. Kampuni inayozalisha maji ya Kilimanjaro, Bonite Bottlers Ltd haijatangaza nafasi zozote za kazi.

Tunaendelea na uchunguzi kubaini chanzo/vyanzo vya taarifa hizi na hatua kali za kisheria zitachukuliwa pindi tutakapobaini wahusika, kampuni hiyo ilifafanua katika tangazo lake la jana.

■**Angalia kwenye tangazo hapo chini kupata taarifa zaidi.**

KILIMANJARO DRINKING WATER
P.O.BOX 205 MOSHI INDUSRIAL AREA
KILIMANJARO
TANZANIA.

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA VIJANA WA KITANZANIA**

Kiwanda cha kutengeneza na kuzalisha maji safi na salama ya kunywa **KILIMANJARO DRINKING WATER**. Kinapenda kutangaza nafasi za ajira kwa vijana wa Kitanzania 543.

Kiwanda kimeongeza kasi ya uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hadi nje ya mipaka ya Tanzania, hivyo ni wazi kuwa kiwanda kinahitaji Rasilimali watu ili kumudu kasi ya uzalishaji.

**NAFASI ZINAZO HITAJIKA NA SIFA ZA MWOMBAJI.**

1. Wafanya kazi ndani ya kiwanda katika vitengo mbalimbali ikiwemo uzalishaji (**NAFASI 425)**
2. Wahasibu (**Nafasi 22**)
3. Viongozi wasimamizi (**Nafasi 5**)
4. Fundi umeme wa viwandani (**Nafasi 16**)
5. Walinzi (**Nafasi 15**)
6. Wafanya usafi (**Nafasi 10**)
7. Dreva wa magari makubwa na madogo (**Nafasi 25**)
8. Wasambazaji (watakuwa wana ambatana na madreva ) **Nafasi 25**
9. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usio pungua miaka 18 na usio zidi miaka 45
10. Mwombaji awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea

FAKE

Mwombaji aambatanishe nakala zake zote (elimu, cheti cha kuzaliwa na leseni) Barua ya maombi ya kazi ikiainisha aina ya kazi anayo omba pamoja na CV.
Maombi ya kazi yatumwe kwenda kwa Afisa Mwajiri (HR) kupitia email hizi. hrkilidrinkingwater@gmail.com au hrkilimanjarowaters@gmail.com
Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **24/03/2022**
Waombaji walio kidhi vigezo tu ndio wata julishwa kuhusu kupokelewa kwa maombi yao

IMETOLEWA NA HR
KILIMANJARO DRINKING WATER

KILIMANJARO DRINKING WATER
P.O.BOX 205 MOSHI INDUSRIAL AREA
KILIMANJARO
TANZANIA.

**WITO KWA AJILI YA USAILI**

Ndugu, asante kwa maombi ya kazi, tumezipitia nyaraka zote ulizo tutumia tumejiridhisha kuwa unaweza kutufaa kwa ajili ya kazi; Hivyo tunakuhitaji kwa ajili ya kufanya usaili.

Usaili utafanyika kwa awamu mbili maana bado tunaendelea kuchambua pia maombi yanayo endelea kutumwa hadi mwisho utakapo fika.

Umechaguliwa katika awamu ya kwanza ya usaili ambayo itafayika kwa siku mbili tarehe. **18 & 19/03/2022.**
Usaili utafanyika katika vituo viwili tofauti. Kituo cha kwanza ni ukumbi wa **VETA HOTEL** uliopo **DODOMA** kituo cha pili ni ukumbi wa **NEW CASTLE** uliopo **MOSHI MJINI.**

Kwasababu ya idadi kubwa ya wasailiwa tumeamua kufanya kwa siku mbili mfululizo. Hivyo wote walio chaguliwa kwa ajili ya usaili watatakiwa kuripoti katika kituo cha usaili tarehe **17/03/2022**, hii ni pamoja na wale wanao ishi ndani ya Mkoa wa Dodoma au Moshi.
Kwa siku zote mbili chakula na malazi vitakuwa katika hoteli zilizo andaliwa kwa ajili ya wasailiwa.

FAKE

Unatakiwa kuthibitisha uwepo wako mapema kwa kulipia pesa kwa ajili ya malazi na chakula ambayo ni **TSH. 35,000/=** kwa siku zote mbili.
Watakao faulu usaili watapewa wiki moja kwenda kujiandaa kisha watatakiwa kuripoti katika kituo cha kazi.

Malipo yatumwe kwa mhasibu kupitia namba **0 657 853 643 MAHAMUDU SIKALUZWE**. Baada ya kufanya malipo tuma majina yako matatu, kituo utakacho fanyia usaili pamoja na sms ya malipo kwenda kwa mhasibu kupitia email hii mhasibukiliwaterdrinks@gmail.com
Watakao shindwa kuthibitisha uwepo wao nafasi zao watapewa watu wengine.

IMETOLEWA NA HR
KILIMANJARO DRINKING WATER



Balozi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Edo Kumwembe, akihakiki stempu katika moja ya maduka ya vinywaji mjini Babati mkoani Manyara mwishoni mwa wiki: **PICHA: TRA**

# Balozi wa kodi ahimiza uhakiki wa stempu

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

BALOZI wa Kodi, Edo Kumwembe, amewataka wafanyabiashara wa vinywaji na watumiaji wa vinywaji hivyo kuwa na utaratibu wa kuhakiki vinywaji kwa kutumia app maalumu ya "Hakiki Stempu" ili kutambua bidhaa feki sokoni ambazo zina athari kwa mlaji.

Akizungumza mjini Babati mkoani Manyara mwishoni mwa wiki, Balozi Kumwembe alisema app ya Hakiki Stempu ina uwezo wa kutambua uhalali wa bidhaa za vinywaji ambazo zipo sokoni.

Alisema mtumiaji atapaswa kuwa na app hiyo katika simu janja na kufanya uhakiki kwa kutumia simu yake iwapo bidhaa hiyo inafaa kwa matumizi ya binadamu.

Balozi wa Kodi huyo alisema kuwa baada ya kupakua app hiyo, mtumiaji atapata njia mbili za kuhakiki stempu kwenye vinywaji.

Alifafanua kuwa njia ya kwanza ni kuingiza tarakimu (namba) zinazoonekana kwenye stempu zisizopungua nane (8) na njia ya pili ni kupiga picha (scanning) tarakimu/namba zinazoonekana kwenye stempu.

Kumwembe alisema lengo la kuhakiki ubora wa bidhaa za vinywaji ni kuhakikisha mlaji anatumia bidhaa bora kwa afya yake.

Vilevile, alisema uhakiki wa stempu unasaidia kuongeza mapato ya serikali kwa kuhakikisha stempu iliyo kwenye bidhaa hiyo ni sahihi kuendana na aina ya bidhaa husika.

Alisema kuwa kwa kutumia mfumo huo wa app, mtumiaji wa bidhaa atapata taarifa sahihi kuhusu mzalishaji wa bidhaa, ujazo wa bidhaa na lini itaisha muda wake.

Muuzaji wa vinywaji mbalimbali mjini Babati, Naingwa, aliipongeza Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kutoa elimu juu ya matumizi sahihi app hiyo inayoweza kuhakiki ubora na uhalali wa vinywaji na kwamba itawasaidia kuepuka kununua bidhaa feki. "App hii ina faida nyingi kwetu wafanyabiashara hasa pale tunapokwenda kununua vinywaji kwani itatusaidia kutambua vinywaji feki pamoja na kufahamu ubora wa vinywaji hivyo ili kumlinda mteja," alisifu.

Maofisa wa TRA kutoka Makao Makuu wako mkoani Manyara kwa siku 10 katika kampeni ya Elimu ya Kodi Mlango kwa Mlango inayolenga kutoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara juu ya matumizi sahihi ya risiti za kielektroniki (EFD), wajibu na haki za mlipakodi pamoja na kusikiliza kero zinazowakumba katika ofisi za TRA pindi wanapokwenda kupata huduma.

# Wadau wa mazingira wasifu sera mpya

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa mazingira nchini wameishukuru serikali kwa kuipitia na kuiboresha sera ya mazingira na kuja na sera mpya ya mwaka 2021 ambayo inaendana na mazingira ya sasa.

Akifungua mdahalo kuhusu mchango wa sekta binafsi katika utunzaji wa mazingira jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Mtandao wa Maendeleo Endelevu (SDN), Freddy Kwezi, alisema sera hiyo inawaongoza wadau katika utekelezaji wa utunzaji mazingira nchini.

"Ninaipongeza serikali kwa kutuletea sera hii mpya ambayo imeongeza mambo mengi yanayoendana na mabadiliko ya kimazingira hasa kutokana na ukuaji wa teknolojia, kwa kutoa mwongozo uliorahisisha utendaji kazi wetu katika suala zima la utunzaji wa mazingira," alisema Fred.

Meneja Opereshieni katika kampuni ya ukusanyaji taka ya Bin Master Limited, Asumini Gombo, alisema kuwapo kipengele cha udhibiti wa taka katika sera hiyo kumefungua ushirikiano na serikali katika kudhibiti kuzagaa kwa taka mitaani.

"Kama wadau wa taka tulikuwa tukipiga kelele kuwapo na sera inayohusu udhibiti wa taka. Ninashukuru sera mpya imeturahisishia na kutufungulia mlango wa kufanyia kazi suala hili," alisema Asumini.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mazingira ya HUDAFO, Sarah Pima, alisema serikali kwa kuweka kipengele cha teknolojia, kutawaongoza utekeleza majukumu yao bila uoga na kusaidia nchi katika kutunza mazingira.

Mhandisi Kyaruzi Boniface licha ya kuishukuru serikali kwa kuboresha sera hiyo, alisema ina upungufu kadhaa ambao serikali inabidi iufanyie kazi kabla ya sera hiyo kuwa sheria.

Alibainisha baadhi ya upungufu huo ni suala la taka hatarishi kutoongelewa kwa kina katika sera hiyo, hali inayoleta ugumu kwa wadau katika kufanyia kazi udhibiti wa vifaa hivyo.

"Ninapoongelea taka hatarishi, ninamaanisha vifaa vya hospitalini kama vile sindano, viwembe, dawa zilizopita muda wake, ambavyo vikitupwa mahali halafu kwa bahati mbaya mtu akakatwa na kifaa hicho anaweza pata maambukizi, hili lilipaswa kuchambuliwa udhibiti wake kwenye sera," alishauri.

Aliitaja upungufu mwingine ni kutokuainishwa kwa makundi maalumu katika sera ambayo kwa uhalisia ndiyo wahusika wakuu wa utunzaji wa mazingira.

"Ninaipongeza serikali kwa kuwatambua wanawake kwenye sera katika utunzaji wa mazingira, lakini kuna makundi ya wanawake, watu wenye ulemavu na wazee wapo mstari wa mbele katika utunzaji wa mazingira, serikali ingefafanua ujumuishi wa makundi haya katika sera," alishauri.

Veronica Korela, Mwendesha Sera katika Taasisi ya Nipe Fagio, alishauri kuwapo kwa sera ya usimamizi wa taka ngumu inayojitegemea kwa kuwa jambo hilo linaonekana kuwa sugu nchini.

"Ninafikiri serikali ingetunga sera ya usimamizi wa taka ngumu inayojitegemea, ifafanue kwa kina ikiwamo kuijengea jamii utayari wa kudhibiti taka katika ngazi ya familia, kwa sababu taka ngumu zimekuwa tatizo sugu na kwa kweli kuna maeneo hayaangaliki mara mbili kutokana na kujaa kwa taka hizi," alisema Veronica.

## TAWIA yatekeleza mwongozo wa kukabili UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Wajane Tanzania (TAWIA) kimesema kinasimamia hatua zote zinazoelekezwa na mwongozo wa Wizara ya Afya kuhusu kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 kwa ajili ya usalama wa afya za wanachama wake.

Mkurugenzi wa chama hicho, Rose Sarwat, aliiambia Nipashe juzi kuwa kila mwanachama wa TAWIA ameelekezwa kuwa na ndoo ya maji tiririka, vitakasa mikono na barakoa nyumbani kwake na kuvitumia.

"Tunazingatia mwongozo huo kuanzia nyumbani hata ofisini kwetu kuna huduma hiyo pia. Ni lazima mgeni anawe mikono kwa maji tiririka na ni lazima awe amevaa barakoa ndipo aingie ofisini," alisema Rose.

Aliongeza kuwa lengo la chama hicho kuweka wajane pamoja ni kutambuana, kufahamiana, kujua vikwazo mbalimbali wanavyopitia na kutafuta njia kuvitatua.

Alisema wamekuwa wakisaidiana kusomesha watoto, elimu ya sheria, afya, saikologia, biashara na ujasiriamali, pia kushirikiana na taasisi nyingine kutoa elimu kwa jamii iiwatambue wajane, kuwapenda, kuwathamini na kuwasaidia kwa hali na mali.

Rose alisema chama hicho pia kinasimamia sheria inayotetea haki za mjane Tanzania, ikiwamo hati ya mirathi na usimamizi wa mali za familia baada ya kifo cha mume na kurejesha matumaini mapya kwa mjane na wajane watarajiwa.

"Pamoja na hayo, hatuwezi kuwa kimya kuhusu corona, ndiyo maana tunahimiza wanachama wetu kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya ambao unaelekeza kuchukua hatua hizo za kujikinga na ugonjwa huo," alisema.

Akizungumzia kuhusu chanjo, mkurugenzi huyo alisema hilo ni suala la hiari ya mtu binafsi ambalo kila mmoja anatakiwa kuamua mwenyewe kwenda kuchanja au kubaki bila kupata huduma hiyo.

"Kwa hiyo mwanachama awe amechanja au bado, tunataka kuhakikisha anazingatia mwongozo wa wizara, na huwa tunawatembelea wanachama wetu kuwajulia hali, lakini pia kuangalia kama wanazingatia mwongozo," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Dk. John Mduma (wapili kushoto), akiwa na baadhi ya wadau waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), katika mkutano huo uliofanyika Mjini Unguja, Visiwani Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WCF yawataka waajiri watumie fursa iliyoko

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umewahimiza waajiri nchini kuchangamkia fursa ya punguzo la michango lililotolewa na serikali kuanzia Julai Mosi, 2021 ili kulinda nguvu kazi na kuongeza ari ya wafanyakazi wao.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Dk. John Mduma, alitoa rai hiyo alipozungumza na wahariri baada ya Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) 2022 uliofanyika mjini Unguja.

Dk. Mduma alisema kuwa katika mafanikio ya siku 365 za Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, WCF inajivunia kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kwa kukubaliwa kutoa punguzo la uchangiaji kutoka asilimia moja kwa waajiri wa sekta binafsi hadi kufikia asilimia 0.6 na punguzo la riba ya madeni ya nyuma ya michango kwa sekta zote kutoka asilimia 10 mpaka asilimia mbili (2).

Alifafanua kuwa moja ya wajibu wa WCF ni kulinda nguvu kazi ya wafanyakazi kuanzia matibabu ya mfanyakazi aliyepata ajali au ugonjwa kutokana na kazi ili kuwawezesha waajiri kuendelea kusimamia uzalishaji wakati wafanyakazi wao wakiendelea kuhudumiwa na WCF.

"Ninakushukuru sana Mwenyekiti wa TEF kwa kutupa nafasi hii ya kushiriki kwenye hadhira hii ambayo kimsingi inatuwezesha kuufahamisha umma kuhusu WCF inavyowajibika katika kulinda nguvu kazi ya Tanzania.

"Tunapenda kuwahimiza waajiri wa sekta binafsi kuchangamkia fursa hizi za uboreshaji ikiwamo punguzo la uchangiaji na tozo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati yao na wafanyakazi," alisema Dk. Mduma.

Alibainisha kuwa WCF inashirikiana kwa karibu na Taasisi ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ikiwamo kubadilishana mawazo na kupeana uzoefu juu ya masuala ya fidia kwa wafanyakazi.

"Sisi kama wabobezi karibu miaka saba sasa ya utekelezaji wa Sheria ya Malipo ya Fidia kwa Wafanyakazi, tumekuwa tukipeana uzoefu na kujadiliana nao ili nao waweze kuelekea kwenye upande huo," alisema.

Mtaalamu wa Takwimu wa WCF, James Tenga, aliwajulisha wahariri kuhusu masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya mfuko huo ikiwa ni pamoja na taratibu za madai ya fidia kwa mfanyakazi anapoumia, kuugua au kufariki dunia kutokana na kazi ili kulipwa fidia.

Pia alisisitiza umuhimu wa waajiri kujisajili katika mfuko na kuwasilisha michango ya kila mwezi ambapo kwa sasa huduma zote za mfuko huo hutolewa kwa njia ya mtandao ikiwamo uwasilishaji wa madai.

Mkutano Mkuu wa TEF, 2022 ulifunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Unguja, Zanzibar.


### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
### TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'

**1. UTANGULIZI:**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu katika Manispaa ya Morogoro na tawi Mkoani Mbeya. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa kimepanga kuendesha kozi mbali mbali za kujenga/kuimarisha uwezo wa kiutendaji kazi. Hivyo, inawatangazia watu wote wenye sifa na nafasi za kushiriki mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kutuma maombi kwa Kozi zifuatazo: -

| SN | JINA LA KOZI | MUDA WA MAFUNZO | KITUO CHA MAFUNZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Matumizi ya software ya 'MS Project' katika kufanya makadilio ya Gharama za Ujenzi ('Application of Microsoft Project software for Project Cost Estimation') | Siku tano (5) 04/04/2022 – 08/04/2022 | **Mkoani Morogoro katika Chuo cha ICoT – Morogoro** |
| 2 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)** 11/04/2022 – 17/06/2022 | **Mkoani Mbeya katika Chuo cha ICoT – Mbeya** |
| 3 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)** 11/04/2022 – 17/06/2022 | **Mkoani Morogoro katika Chuo cha ICoT – Morogoro** |

**2. MAADA / MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

**(a) Kozi ya 'Application of Microsoft Project software for Project Cost estimation'**
Katika kozi hii, washiriki watajifunza mambo mbalimbali juu ya kutengeneza mradi, kuingiza rasilimali za mradi, kufanya makadilio ya gharama za mradi,na kufuatilia maendeleo ya mradi katika hatua mbali mbali kwa kutumia 'software' ya 'Microsoft Project'.

**(b) Kozi ya ukarabati na matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe**
Washiriki watajifunza mambo mbalimbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Pia, watajifunza mambo mbalimbali juu ya; mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa tabaka la changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati.
Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe/ udongo kwa ubora wa hali ya juu.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**

Mafunzo yatafanyika kwa nadharia na kwa vitendo. Mafunzo ya nadharia katika kozi ya Matumizi ya software ya 'MS Project' katika kufanya makadilio ya gharama za ujenzi ('Application of Microsoft Project software for Project Cost estimation'), yataambatana na vitendo katika muda wote wa mafunzo. Kozi imesajiliwa na ERB hivyo washiriki watapata 'PDUs'.

Katika kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi, mafunzo ya nadharia (darasani) yatafanyika kwa muda wa wiki nne (4) na mafunzo ya vitendo (site) yatafanyika kwa muda wa wiki sita (6).

**4. MALENGO YA KOZI**

Malengo ya kozi ya Matumizi ya software ya 'MS Project' katika kufanya makadilio ya gharama za ujenzi ('Application of Microsoft Project software for Project Cost estimation') ni kama ifuatavyo: -

i. Kuwapatia washiriki ujuzi wa kutumia 'software' ya 'MS Project' katika kukadilia gharama za miradi;
ii. Kuwajengea/kuwaimarishia uwezo washiriki katika kufanya kazi za kuendesha, kusimamia na kufuatilia maendeleo ya miradi kwa urahisi na ufanisi zaidi kwa kuwapa ujuzi wa matumizi ya 'software ya 'MS Project' katika kazi za miradi; na
iii. Kuwaongezea sifa za ushindani katika soko la ajira.

Maada zitakazofundishwa katika kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yanalenga kumpatia mshiriki mbinu mbalimbali juu ya matumizi ya Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinayotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

(a) Walengwa wa kozi ya Matumizi ya software ya **'MS Project'** katika kufanya makadilio ya gharama za ujenzi **('Application of Microsoft Project software for Project Cost estimation')** ni: -
i. Mameneja wa miradi,
ii. Wahandisi wote kutoka sekta ya Umma na binafsi,
iii. Mafundi Sanifu wanaofanya kazi za usimamizi wa miradi kutoka sekta ya Umma na binafsi,
iv. Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
v. Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo / ukarabati wa barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
vi. Watu binafsi wenye uzoefu katika matumizi ya kompyuta na wanaohitaji kujua matumizi ya 'software' ya 'MS Project'.

(b) Walengwa wa kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ni: -
i. Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
ii. Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
iii. Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
iv. Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
v. Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**

Lugha itakayo tumika kufundishia katika kozi zote ni Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:
i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 900,000; na
ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.

b) Kozi ya matumizi ya software ya '**MS Project'** katika kufanya makadilio ya gharama za ujenzi **('Application of Microsoft Project software for Project Cost estimation'):**
Gharama za kozi hii ni shilingi za Tanzania 500,000 (Laki tano tu) ambayo itagharamia mafunzo yenyewe, chai ya asubuhi na chakula cha mchana tu katika kipindi chote cha mafunzo.
Aidha, ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**Muhimu:**

1. Washiriki wa kozi ya Matumizi ya software ya 'MS Project' katika kufanya makadilio ya Gharama za Ujenzi ('Application of Microsoft Project software for Project Cost Estimation') wanatakiwa kuja na kompyuta zao kwa ajili ya kufanyia mazoezi yatakayotolewa wakati wa mafunzo.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA TAASISI**

**Institute of Construction Technology ICoT,**
**S.L.P 963, MOROGORO.**
**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**
**: 0762 409087/0786 384 062**
**Nukushi : 023-2935227**
**Barua pepe : mwti@morogoro.net**

**Institute of Construction Technology ICoT,**
**S.L.P 1957, MBEYA.**
**Simu : 025 295 7484/5**
**: 0787 059 555/0769 317 404/0765 251 509**
**Nukushi : 025 295 7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

216747502

# Ukimwona kijana huyu, toa taarifa



**Na Mwandishi Wetu**

KULWA Samweli (35) (pichani), mkazi wa Kijiji cha Magu wilayani Magu, amepotea baada ya kwenda matembezi Machi 9, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, dada yake, Joyce Safi, alisema mdogo wake huyo ana matatizo ya akili na amekuwa akitoka nyumbani na kwenda kutembea mitaani kisha kurudi nyumbani.

"Siku ya tukio majira ya saa 11 jioni, alitoka kama kawaida yake, tukajua hayuko mbali, lakini tukashangaa muda unazidi kwenda na harudi nyumbani. Tukaanza kumtafuta bila mafanikio mpaka leo hii," alisema.

Aliongeza kuwa siku ya tukio mdogo wake huyo alikuwa amevaa jezi ya Chelsea ya rangi ya bluu yenye namba 16 mgongoni, suruali 'track' na yebo nyeusi.

Alisema kuwa baada ya kumtafuta bila mafanikio walitoa taarifa Kituo cha Polisi Wilaya ya Magu na kufungua jalada lenye namba RB 467.

Joyce alisema yeyote atakayemwona, atoe taarifa kituo cha polisi kilichoko karibu au apige simu kwenda namba **0689093032 au 0785158694.**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akisalimiana na Meya wa Ubungo, Jaffary Nyaigesha, katika ziara ya mameya wa mkoa wa Dar es Salaam kutembelea ofisi za Benki ya NMB jijini humo. Msafara huo wa mameya uliongozwa na Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ataka usimamizi miradi ya bilioni 38/-

**Na Christina Haule,** KILOSA

MKUU wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro amewaagiza wananchi, viongozi wa kata na halmashauri kuhakikisha wanasimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 38 zilizotolewa na serikali.

Alhaji Majid Mwanga aliagiza hayo juzi wakati wa sherehe za kuelekea mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani zilizofanyika wilayani humo.

Kiongozi huyo alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa zilizopewa fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani.

Alisema fedha hizo zimetumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwamo ya barabara, minara 12 ya simu katika vijiji mbalimbali ambavyo vilikosa huduma ya simu na madarasa yaliyojengwa kwa fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema kuwa bila usimamizi kwenye utekelezaji huo, hawatafikia malengo ya kumuunga mkono Rais Samia, hivyo akawataka wananchi kuhakikisha wanashiriki vya kutosha katika miradi ya serikali ukiwamo unaoendelea wa anwani za makazi.

Alisema itakuwa ni aibu kama vibao vitakavyowekwa katika mitaa yao kwa ajili ya kutambulisha mitaa na nyumba zao wakavikuta kwa wauzaji wa vyuma chakavu.

Mkuu wa Wilaya alitoa angalizo kwa wale wenye nia ya kuiba na kuuza miundombinu hiyo kama vyuma chakavu kuwa serikali haitawafumbia macho.

Mwanga pia aliwataka wananchi kuhakikisha wanapata chanjo ya UVIKO-19 na kujitokeza kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itayosaidia kujua mabilioni ya fedha walizopata mwaka huu yanatosha au hayatoshi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Pia aliwahimiza wananchi kumuunga mkono Rais Samia kwa kupanda miti mitano kwa kila kaya (mitatu ya matunda na miwili ya kivuli).

Alisema wazazi, viongozi wa vijiji, vitongoji na kata wanapaswa kuhakikisha watoto wote wasioenda shuleni wanaenda shuleni kwa kuwa hadi sasa karibu asilimia 16 ya watoto wote wanaotakiwa kwenda kidato cha kwanza wilayani humo bado hawajaripoti shuleni.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo, Amer Mubarak, aliiomba serikali kuwasaidia kupata vivuko katika reli ya mwendokasi ambavyo vilikuwa vikipatikana zamani ili kuwapunguzia kero ya ajali za mara kwa mara.

Awali Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi, aliishukuru serikali kwa kujali maisha ya watu wa kawaida kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miundombinu ya madaraja kuunganisha kata kwa kata na tarafa kwa tarafa likiwamo daraja kubwa la Mto Mkundi kwenye Kata ya Berega.

Alisema Mji wa Kilosa ndio utakaokuwa kiungo cha usafiri baada ya muunganiko wa barabara za kati ya mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Zambia, Congo ya Mashariki na Malawi.

# Benki ya TCB yazindua tawi la 6 mkoani Arusha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) imekipandisha hadhi kituo cha huduma cha Usa River wilayani Arumeru kuwa tawi kamili na kufanya taasisi hiyo kongwe ya fedha nchini kuwa na jumla ya matawi sita katika Mkoa wa Arusha.

Tawi hilo jipya lilizinduliwa rasmi Ijumaa wiki iliyopita na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, aliyeipongeza benki hiyo kwa kuongoza ajenda ya taifa ya huduma jumuishi za fedha.

Kiongozi huyo alisema kupandishwa hadhi kwa kituo cha Usa River ni ushahidi mwingine wa dhamira ya TCB kuzipeleka huduma zake karibu na wananchi na kushiriki kiamilifu katika ujenzi wa taifa.

Mongela aliwahimiza wananchi wa eneo hilo, hasa wanawake, kutumia fursa hiyo kuboresha maisha yao na kuchochea shughuli za uzalishaji mali. Alisema Mkoa wa Arusha utaendelea kuwa karibu na TCB na kufanya kazi na benki hiyo kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Awali Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, alisema kituo hicho kilichokuwa kwenye ofisi za Shirika la Posta (TPC) kimepandishwa daraja kutokana na kufanya vizuri kibiashara na kukua kwa shughuli zake.

"Benki yetu imepata mafanikio makubwa na kwa sasa Tawi la Usa River lina jumla ya wateja 5,916 wanaofurahia huduma mbalimbali za kibenki hususani mikopo yenye riba nafuu kama ya kilimo, biashara, watumishi na wastaafu pamoja na kufanya miamala mbalimbali ya kifedha ndani na nje ya nchi," Moshingi alibainisha.

Aliongeza: "Kwa kipindi cha mwaka 2020 mpaka February 2021, tawi limeweza kutoa mikopo ya kiasi cha Sh. bilioni 5.78 kwa wadau mbalimbali. Kukua kwa biashara kumefanikisha benki kuhama kutoka katika ofisi ndogo za TPC na kuhamia katika jengo jipya tunalolizindulia leo lenye nafasi kubwa na kuwezesha kutoa huduma kwa ubora na umahiri zaidi."

Matawi mengine ya TCB mkoani Arusha ni ya Meru, Kwamorombo, Mto wa Mbu, Sokoine na Tanzanite. Tawi la Usa River ni la nne kufunguliwa na benki hiyo mwaka huu baada ya uzinduzi wa yale ya Kigamboni, Mpanda na Mbinga yaliyoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Katavi na Ruvuma mtawalia.

Moshingi alisema tawi hilo lina wafanyakazi 12 wanaosaidiwa na mawakala 60 kuihudumia wilaya hiyo. Aliongeza kuwa TCB pia ipo mstari wa mbele kwenye shughuli za kijamii kwa kutoa misaada mbalimbali.

"Ni matarajio yetu kuwa biashara itaendelea kukua na kutuwezesha kufungua matawi katika kila wilaya ili kuwezesha bidhaa na huduma zetu kuwawafikia Watanzania wote kwa ukaribu zaidi," Moshingi alisema.

Kiongozi huyo alisema TCB pia imepata mafanikio makubwa kiubunifu na kidijitali, akitolea mfano huduma ya kuweka akiba kwenye vikundi ya M-koba. Kwa kushirikiana na Kampuni ya Vodacom tayari wamekusanya zaidi ya Sh. bilioni 27 kupitia huduma hiyo.

"Lakini kikubwa zaidi, benki yetu imefanikiwa kutoa kadi za Visa, hivyo basi wananchi wa Arusha na Tanzania kwa ujumla karibuni sana mjipatie kadi za Visa kwa kufanikisha miamala yoyote popote mlipo," Moshingi alisisitiza.

NIPASHE JUMATATU MACHI 14, 2022
Nipashe
Spotika



KOCHA GANI CHAGUO SAHIHI MANCHESTER UNITED? UK. 12-13




# NYOTA WA5 WALIOKO KWENYE KIWANGO BORA EPL KWA SASA

## ISIKUPITE

HAT-TRICK aliyofunga Cristiano Ronaldo wakati Manchester United ikishinda 3-2 dhidi ya Tottenham Hotspur juzi, ni ya kwanza kwake kwenye Ligi Kuu England baada ya miaka 14 na siku 59, mara ya mwisho kwa nyota huyo wa Ureno kufunga mabao matatu katika ligi hiyo ilikuwa katika ushindi wa 6-0 dhidi ya Newcastle United mwaka 2008.



**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu England 2021-22, umekuwa wa kufurahisha, huku mbio za nne bora za juu na kushuka daraja zikishika kasi.

Mbio za taji pia ziko wazi. Lakini pengo kati ya vita hivi vingi limepunguzwa kwa sababu ya wachezaji fulani, ambao wamepata kiwango kizuri hivi karibuni.

Ligi Kuu England (EPL), ina baadhi ya wachezaji wasio na kiwango kikubwa barani Ulaya kwa sasa.

Msimu wa sasa wa ligi hiyo umekuwa hautabiriki, huku nyota kadhaa wakiwa nje ya kiwango chao cha mwanzoni mwa msimu. Lakini, sasa wanakuja kivyao, na pia kuna seti nyingine ya wachezaji ambao wamekuwa thabiti katika kipindi kizima cha msimu.

Lakini jambo la sasa ni muhimu zaidi, na wachezaji ambao wanapiga hatua wanaweza kuthibitisha katika nne bora, sita bora na mbio za ubingwa.

Kwa maelezo hayo, tunawaangalia wachezaji watano walio katika kiwango bora zaidi kwenye Ligi Kuu hiyo kwa sasa - Machi 2022, hawa hapa...

### #5. ORIOL ROMEU

Oriol Romeu amekuwa na kipaji katika mwezi mmoja uliopita akiwa na Southampton. 'Watakatifu' hao walikuwa kwenye nafasi ya kati katika msimamo wa Ligi Kuu hadi mwezi uliopita, lakini sasa wanaonekana kukimbilia kwenye sita bora.

Kocha Ralph Hasenhuttl ni mtaalamu wa kutengeneza wachezaji bora zaidi kutoka kwa wachezaji wake na amefanya hivyo hivyo na Romeu katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita. Kiungo huyo alipitisha mpira kwa utulivu huku pia akitoa ulinzi wa kutosha kwenye safu yake ya nyuma.

Alimaliza mwezi wa ajabu kwa kufunga katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Norwich mwishoni mwa Februari.

Iwapo Romeu ataendelea hivyo, kikosi hicho kitakuwa kila nafasi ya kumaliza katika nafasi sita za juu msimu huu.

### #4. JAMES WARD-PROWSE

Kutoka kwa mchezaji mmoja wa Southampton hadi mwingine, James Ward-Prowse ameendelea kuthibitisha umuhimu wake kwa klabu hiyo msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, anacheza kwa hamu nyingi na huweka kila kitu uwanjani wiki baada ya wiki.

Mikwaju ya faulo iliyotiwa saini na Ward-Prowse karibu kila mara inalenga lango isipokuwa kama golikipa wa timu pinzani ataweza kuokoa hatari.

Alidhihirisha ubora wake kutokana na pasi zake mbili za haraka katika ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Tottenham Hotspur mapema Februari. Akiwa na mabao sita na asisti nne kwa jina lake, Ward-Prowse amekuwa na uthabiti wa hali ya juu katika Ligi Kuu msimu huu.

### #3. JOAO CANCELO

Joao Cancelo amekuwa beki wa pembeni bora zaidi kwenye Ligi Kuu England msimu huu. Mchezaji huyo wa Ureno alikuwa na mwisho mzuri msimu uliopita na amekuwa kwenye kiwango cha juu katika misimu yote ya sasa.

Ingawa viungo wa kati wa Manchester City wameajiriwa na kazi ya kutengeneza mabao, Cancelo amejitwika jukumu la kushambulia kila mara na kutoa mchango wa kushambulia. Lakini hiyo haimaanishi kuwa amesahau kazi yake ya ulinzi kwani ana akili sana katika suala hilo pia.

Ingawa hakuwa na mchango wowote wa mabao kwa mwezi uliopita, alikuwa sehemu ya safu ya ulinzi iliyoruhusu bao pekee katika mchezo mmoja kati ya mechi tatu za Ligi Kuu England.

Cancelo ana bao moja na asisti tano kwenye ligi msimu huu, lakini anaweza kuongeza idadi hii kutokana na kiwango chake cha moto.

### #2. HEUNG-MIN SON

Heung-min Son amekuwa mmoja wa mawinga bora zaidi kwenye Ligi Kuu katika miaka michache iliyopita. Raia huyo wa Korea Kusini amekuwa kwenye kiwango chake bora akiwa na Tottenham Hotspur.

Wakati wachezaji wachache sana walihamasishwa na uteuzi wa kocha Nuno Espirito Santo, Son alifanikiwa chini yake.

Mambo yameendelea kuwa sawa chini ya Antonio Conte na winga huyo amekuwa bora zaidi katika miezi michache iliyopita akicheza kwa upatina mzuri na Harry Kane.

Wawili hao wamekuwa hatari kwenye shambulio la kujibu mashambulizi na nyota huyo wa Asia amekuwa akipenya safu ya ulinzi ya upinzani kwa urahisi.

Son alifunga mabao mawili Februari na sasa ana mabao 10 ya ligi na asisti tano msimu huu, akionyesha uchezaji wake thabiti katika kipindi chote cha msimu.

### #1. HARRY KANE

Harry Kane alikuwa na moja ya mwanzo mbaya zaidi msimu huu. Sakata lake la uhamisho lililoshindikana lilibeba mzigo mkubwa akilini mwake na alishindwa kufanya vema chini ya kocha Nuno Espirito Santo.

Hata hivyo, Antonio Conte ameweza kupata kilicho bora zaidi kutoka kwa nyota huyo wa Spurs. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alikuwa na mabao machache pekee hadi Desemba, lakini amefikisha jumla ya mabao nane kwenye ligi na kutoa asisti tatu.

Umuhimu wake ulionekana katika ushindi wa mabao 3-2 wa hivi karibuni dhidi ya Manchester City, kwani alifunga mara mbili, zikiwamo dakika za nyongeza na kuipa timu yake pointi zote tatu.

Kane ni mmoja wa washambuliaji walio na kiwango kizuri na kila anachogusa hugeuka dhahabu. Mshambuliaji huyo anaweza kuwa sababu ya Tottenham kufanikiwa kutinga nne bora msimu huu.

# KOCHA GANI CHAGUO SAHIHI MAN UNITED?



ERIK TEN HAAG

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United iliyo na nyota wengi bado inashindwa kubadilisha uchezaji wake na kuwa wa ushindi. Wakati mapambano ya uwanjani yakiendelea, pia kuna suala la kuchagua kocha wa kudumu anayefuata.

**Majina kadhaa yanajadiliwa kama ndio yenye nafasi ya kuchukua kazi hiyo. Wakati uvumi huo ukiendelea, hapa kuna mwonekano wa baadhi ya majina maarufu wa nafasi ya kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao. Mmoja wao anaweza kuteuliwa katika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.**

Hapa tunajadili majina ya makocha wakubwa ambao wanatajwa zaidi kuwania nafasi hiyo kipindi cha majira ya joto kinachokuja, twende sasa...

### JE, HAAG ATAKUWA KOCHA AJAYE MAN UNITED?

Erik Ten Haag, kocha wa sasa wa Ajax, ni chaguo maarufu miongoni mwa mashabiki wa Manchester United. Tangu mwaka 2017, Mholanzi huyo amenyakua mataji mawili ya Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, kati ya mashindano matatu kamili ambayo ameshiriki, mataji mawili ya KNBV na Supercup moja.

Katika msimu wa 2021/22, Ajax kwa sasa inaongoza kwenye ligi hiyo kwa pointi mbili zaidi huku ikiwa imebakiwa na mechi 10 kuchezwa.

Haag pia amefanikiwa kuiongoza klabu yake katika fainali nyingine ya Kombe la KNBV, ambayo inatazamiwa kuchezwa dhidi ya PSV Aprili, ambao kwa sasa wamepitwa pointi mbili pekee nyuma ya Ajax kwenye msimamo wa ligi.

Haag anapenda kuichezesha timu yake kupitia kwa mawinga na mabeki wa pembeni, na hilo linazifanya timu anazokutana nazo kuwa kwenye wakati mgumu.

Katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018/19, Ajax walikuja wakiwa pungufu katika mechi zao zote. Hata hivyo, waliwatupa nje Mabingwa Watetezi, Real Madrid na Juventus, kabla ya kufungwa na Tottenham Hotspur kwenye nusu fainali.

Wengi wanaamini kwamba Haag anaweza kuwa kitu kikubwa kinachofuata katika jukumu la usimamizi wa mpira wa miguu. Je, Man United wataweza kumpata katika majira ya joto?

Hilo ni gumu kusema hivi sasa, lakini kumekuwa na taarifa kwamba, Haag anasubiri Man United wampate. Lakini nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao inaweza kuwa jambo muhimu katika uamuzi wake.

### JE, POCHETTINO ATAFANIKISHA MPANGO HUO?

Mauricio Pochettino kwa sasa ameajiriwa katika Klabu ya Paris Saint Germain. Lakini tumeona ripoti nyingi zikionyesha kuwa hana furaha katika klabu hiyo. Raia huyo wa Argentina amejidhihirisha katika Ligi Kuu kwa miaka sita ya kazi yake.

Baada ya kuonyesha kiwango kizuri akiwa Southampton, wakiboresha msimamo wao wa ligi kutoka nafasi ya 14 hadi ya nane, alihamia Tottenham Hotspur, ambako, licha ya kutoshinda taji lolote, alileta uthabiti katika uchezaji wa timu hiyo. Alifanikiwa kumaliza katika nafasi nne bora katika kila msimu aliokaa klabuni hapo, isipokuwa msimu wa kwanza.

Moja ya sababu kuu kwa nini mashabiki wengi wangependa kumwona kwenye dimba la Old Trafford ni uvumi kwamba, anaweza kumleta Harry Kane pale Man United.

Kane alistawi chini ya Pochettino na amekuwa mmoja wa washambuliaji bora barani Ulaya. Haitashangaza iwapo Kane ataamua kuhama na kuungana na Mauricio katika kusaka mataji, ambayo ameshindwa kutwaa hadi sasa.

Pochettino anatumia mtindo wa kushambulia wa uchezaji na msisitizo katika kuweka alama kwa watu ili kuweka shinikizo kwa wapinzani. Safu ya kiungo imara, ambayo inaweza kupiga mpira mbele vizuri, ni muhimu kwa timu za Pochettino kuendeleza mashambulizi.

Imependekezwa kuwa uongozi wa United ungempendelea Pochettino kuliko wagombea wengine wengi. Lakini Pochettino ana mkataba na PSG hadi mwaka 2023 na kuondolewa kwa timu hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora na Real Madrid wiki iliyopita, kuna uwezekano na yeye akatimka.

### JE, UNITED INAWEZA KUMCHUKUA ANCELOTTI?

Carlo Ancelotti hivi karibuni alihama kutoka Everton na kurejea Real Madrid ambako amefurahia ushindi mwingi siku za nyuma. Ancelotti ni mmoja wa makocha waliofanikiwa zaidi duniani, akiwa ameshinda Kombe la Klabu Bingwa Dunia la FIFA mara mbili, mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, matatu ya UEFA Super na taji moja la Ligi Kuu.

Pia ana sifa ya kunyakua mataji katika ligi tatu za Ulaya, Serie A, Ligue 1, na Bundesliga. Ancelotti pia ameshinda mataji mengi ya ligi ya ndani katika nchi tofauti barani Ulaya.

Zaidi ya hayo, inadaiwa kuwa kuwa Sir Alex Ferguson amependekeza jina la Ancelotti kwa viongozi wa juu wa Man United kama kocha anayewezekana kwa klabu hiyo.

Kukutana tena na Cristiano Ronaldo kunaweza kuwa pendekezo la kuvutia kwa Muitaliano huyo, ikizingatiwa kwamba alijaribu kumrudisha kwenye dimba la Santiago Bernabeau msimu uliopita wa majira ya joto. Ancelotti amekuwa akijulikana kuwa na mbinu mahiri kulingana na timu anayoifundisha.

Tumeona akitumia zaidi mifumo ya 4-3-2-1, 4-4-2, 4-3-3, na hata 3-5-2 wakati mwingine katika ushambuliaji. Washambuliaji chini ya Ancelotti kwa kawaida hufurahia mafanikio mengi. Tena, kama wagombea wengine wa kazi ya Man United, kutakuwa na mambo mengi ya kuzingatia kwa kocha huyo mkongwe wa soka kabla ya kurejea England.

Haya yote yanaweza kutegemea iwapo Man United itamaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu England msimu huu, au jinsi Real Madrid wanavyosonga mbele kutoka hapa.

## Nukuu

"Rekodi yake ya mabao ni nzuri kwa umri wake wa miaka 37, lakini nadhani kama angejiunga na Manchester City, pengine angekuwa na mabao 25 sasa, kwa sababu wachezaji wazuri huko wangempata kirahisi zaidi, wangekuwa na mbinu ya kumweka ndani, wakati nadhani baadhi ya wachezaji wa Man United hawana maono hayo ya kumweka golini," **Kocha na mchambuzi wa soka, Peter Barnes akiponda uamuzi wa Cristiano Ronaldo wa kutua United badala ya City.**



"Ninakataa kwamba kumekuwa na aina yoyote ya mazungumzo kwa [Erling] Haaland. Nina uhusiano mzuri na [Mino] Raiola, lakini kama ninataka mchezaji, lazima nizungumze na klabu yake," **Rais wa Barcelona, Joan Laporta.**



"Ligi Kuu England ni ligi ngumu duniani, hakuna shaka kwenye hilo, lakini ni changamoto, na hakika tunafurahia, kama tusingekuwapo hapa mwaka huu au miaka miwli iliyopita au mitatu, basi Manchester City angekuwa bingwa Februari," **Kocha wa Liverpool, Jürgen Klopp.**



Nipashe
Spotika



Mwamuzi Emmanuel Mwandembwa, alimwonyesha nahodha wa Ruvu Shooting, Santos Mazengo, kadi nyekundu akiwa kwenye machela, baada ya kumchezea madhambi Fiston Mayele na kuumia mwenyewe kwenye mechi ya Ligi Kuu Novemba 2, mwaka jana. **PICHA: MAKTABA**

# WAAMUZI WALIVYOGAWA UMEME LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

HADI kufika raundi ya 17 ya Ligi Kuu jumla ya wachezaji 13 wameonyeshwa kadi nyekundu kutokana na kufanya rafu na matukio mengine mbalimbali yasiyo ya kiungwana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

**Kwa mujibu wa takwimu zetu na za Bodi ya Ligi, mechi zinazoihusu timu ya Simba ndizo zilizotoa kadi nyingi zaidi kuliko zingine. Jumla ya kadi sita nyekundu imezihusu mechi ambazo Simba imecheza.**

Ni jumla ya timu 10 ambazo wachezaji wao wamezawadiwa kadi nyekundu, huku sita zilizobaki zikiwa hazina mchezaji aliyepewa kadi ya aina hiyo.

Timu sita zilizobaki ambazo wachezaji wake mpaka sasa hawajaonja uchungu wa kadi nyekundu hadi kufikia raundi ya 17 ni Yanga, Azam FC, Geita Gold, Prisons, Biashara United, na Mtibwa Sugar.

Timu za Kagera Sugar na Namungo FC ndizo zinazoongoza kwa kuwa na kadi mbili nyekundu kila moja kwa wachezaji wao wawili.

Uwanja wa Benjamin Mkapa, unaongoza kwa mechi zake kuzalisha kadi nyingi zaidi, ukiwa na kadi tano zilizotolewa kwenye uwanja huo. Katika makala haya tunaangalia wachezaji ambao wameonyeshwa kadi nyekundu, mechi gani na sababu za kupata adhabu hizo, haya sasa...

**#1. ANUARY JABIR (DODOMA JIJI VS SIMBA)**

Anuary wa Dodoma Jiji ndiye mchezaji aliyeweka rekodi ya kuwa wa kwanza kupata kadi nyekundu kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Ilikuwa ni Oktoba Mosi mwaka jana kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, alikula umeme, baada ya kumpiga kiwiko beki wa Simba, Kennedy Juma, mechi ikiisha kwa Simba kushinda bao 1-0.

**#2. JOSEPH MAJAGI (MBEYA KWANZA VS DODOMA JIJI)**

Mchezaji huyu wa Mbeya Kwanza alikula umeme Oktoba 27, mwaka jana kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, baada ya kumpiga kichwa Aushutino Msata wa Dodoma Jiji akiwa hana mpira dakika ya 28 baada ya kutokea sintofahamu kati ya wachezaji wa pande zote mbili, mechi ikiisha kwa suluhu.

**#3. JUMA RAMADHANI (POLISI TANZANIA VS SIMBA)**

Juma alimwekea mguu usoni Bernard Morrison aliyekuwa ndani ya eneo la hatari na kusababisha penalti ambayo iliwekwa wavuni na Rally Bwalya Oktoba 27, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba ikishinda bao 1-0. Ndiyo rafu pekee ya kadi nyekundu iliyozaa mkwaju wa penalti kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**#4. BENEDICT JACOB (COASTAL VS SIMBA)**

Mechi hii ilichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 31, mwaka jana, Benedict akipata kadi nyekundu, ikiwa ni ya pili ya njano, ikitokana na kuupiga mpira kwa makusudi ambao Henock Inonga alikuwa anataka kupiga faulo. Mechi iliisha kwa suluhu.

**#5. HENOCK INONGA (SIMBA VS COASTAL)**

Ni mechi hiyo hiyo aliyopewa kadi Benedict, ndiyo Inonga nayo alipata dakika chache baadaye. Mechi ya Simba dhidi ya Coastal Union iliyochezwa Oktoba 31, mwaka jana ndiyo iliyoweka rekodi ya kutoa kadi mbili nyekundu kwa mchezo mmoja. Inonga alizawadiwa kadi hiyo baada ya kumpiga kichwa Issa Abushehe, aliyemvuta jezi.

**#6. SANTOS MAZENGO (RUVU SHOOTING VS YANGA)**

Ilikuwa Novemba 2, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati Yanga ikicheza dhidi ya Ruvu Shooting na kushinda mabao 3-1. Mazengo alimfanyia rafu Fiston Mayele nje kidogo ya eneo la hatari na kulimwa kadi nyekundu.

**#7. ABDULAZIZ MAKAME (NAMUNGO VS SIMBA)**

Kesho yake, Novemba 3, mwaka jana, kwenye uwanja huo huo wa Mkapa, kingo wa Namungo Makame, naye alikula umeme wa moja kwa moja, baada ya kumrukia miguu miwili kama mcheza kung fu, beki wa Simba, Shomari Kapombe kwenye mechi ambayo iliisha kwa Simba kushinda bao 1-0.

**#8. HAMISI KHALIFA (NAMUNGO VS YANGA)**

Huyu ni mchezaji wa Namungo ambaye alikula umeme Novemba 20, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi katika mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Yanga. Mchezaji huyo aliongoza kupiga penalti iliyotolewa na mwamuzi. Na kwa sababu alikuwa na njano, ilibidi apate nyingine. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

**#9. STEPHEN DUAH (KAGERA SUGAR VS PRISONS)**

Duah wa Kagera Sugar alimchezea rafu ya makusudi Mohamed Mkopi wa Prisons katikati ya uwanja wakiwa peke yao na hawana mpira. Akalimwa kadi nyekundu, huku timu yake ilichapwa bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, mechi ikichezwa Desemba 26, mwaka jana.

**#10. MPOKI MWAKINYUKE (MBEYA CITY VS SIMBA)**

Kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, nahodha wa Mbeya City, Mpoki Mwakinyuke, alikumbana na kadi nyekundu baada ya kumkata mtama straika wa Simba, Chris Mugalu kwenye mechi iliyochezwa Januari 17, mwaka huu. Wakati huo tayari alikuwa na njano aliyoipata kwa kupoteza muda. Simba ilifungwa bao 1-0.

**#11. HAMISI KIIZA (KAGERA SUGAR VS SIMBA)**

Kiiza alipata kadi nyekundu Januari 26, mwaka huu, akiwa na njano moja kwa kosa la kuupiga mpira nje, ikitafsiriwa kwanza kutotii maamuzi ya mwamuzi, pili kupoteza muda. Ilikuwa ni mechi kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera, Simba ikilala kwa bao 1-0. Wengine waliopata kadi nyekundu ni Ismail Gambo wa KMC kwenye mechi dhidi ya Coastal Union na Abuswamad Kassim wa Ruvu Shooting.

**JE, WAJUA?**



NYOTA wa zamani wa Manchester United, Ryan Giggs, ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kuwa na mataji mengi (36) kwa kuitumikia klabu moja, akifutiwa na Lionel Messi wakati akiwa na Barcelona (mataji 35) na Xavi Hernandez (Barcelona) mataji 33.





# Walia kukosa maeneo ya kuzika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATA ya Msalato jijini Dodoma inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa huduma za kijamii ikiwamo eneo la makaburi, hali inayosababisha watu kuzikwa kwenye maeneo ya makazi.

Diwani wa Kata hiyo, Nsudi Bukuku, alibainisha hayo juzi alipozungumza kwenye kikao cha kutatua mgogoro wa ardhi baina ya Jeshi la Magereza na wakazi wa kata hiyo, Kata ya Makutupora pamoja Mbalawala kilichoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka.

Bukuku alisema hali hiyo inatokana na kata hiyo kuzungukwa na taasisi za serikali ikiwamo Jeshi la Magereza, Jeshi la Wananchi (JWTZ) na mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato.

Alisema kutokana na hali hiyo maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya huduma za kijamii kama shule na vituo vya afya yamekosekana. "Ndugu Mkuu wa Mkoa, sisi hapa Msalato tuna kero kubwa sana ya maeneo kwa ajili ya ujenzi wa huduma za kijamii kama vile shule, kituo cha afya pamoja na maeneo kwa ajili ya kuzikana. Hali hii inatulazimu kuzikana kwenye maeneo ya makazi yetu," alilalamika.

Diwani huyo alisema hivi sasa shule ya msingi ambayo walikuwa wakitegemea, eneo lake limechukuliwa na mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege.

"Shule ya msingi ambayo tulikuwa tukitegemea kwa miaka mingi watoto wetu wasome imechukuliwa na mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege, hivyo hivi sasa tunasubiri notisi ya kuondolewa na mpaka sasa hatuna eneo ambalo tunaweza kwenda kujenga shule nyingine, hivyo mkuu wa mkoa tunaomba tupatiwe eneo," alisema.

Bukuku aliongeza kuwa maeneo ambayo walikuwa wanayategemea kujenga huduma za elimu na afya kwa asilimia kubwa yanamilikiwa na Jeshi la Magereza na JWTZ Msalato.

"Haya maeneo ya karibu yote yamechukuliwa na taasisi hizi mbili pamoja na uwanja wa ndege na eneo ambalo wanatupa kwenda kujenga ni mbali, takribani kilomita 15," alisema.

Naibu Waziri wa Kilimo na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema ukosefu wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo katika kata hiyo umekuwa kero kwa wananchi.

"Eneo la Msalato ni kata ambayo imebahatika kuwa na miradi mikubwa ya kimaendeleo lakini hivi sasa kumekuwapo na changamoto ya ukosefu wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa huduma za kijamii kama vile shule na vituo vya afya na hata maeneo ya maziko," alisema.

Mavunde alisema serikali imetoa Sh. milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi, lakini eneo walilopatiwa kwa ajili ya kujenga shule hiyo itawalazimu wanafunzi kutembea umbali kilomita 15 kila siku kinyume cha sera ya elimu inayotaka huduma kama hizo kuwa eneo la karibu na jamii.

Akijibu hoja hizo, Mkuu wa Mkoa (Mtaka) alisema amepokea malalamiko ya pande zote na atayawasilisha katika mamlaka zinazohusika ili kupata ufumbuzi.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kushoto), akiwaonyesha wageni wake jinsi walivyofanya ubunifu wa vyumba vitakavyotumiwa na wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kwenye mradi wa soko jipya la Wamachinga lilinalojengwa eneo la Bahi Road jijini Dodoma mwisho wa wiki, wageni kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Iringa, Arusha, Songwe na Mwanza walitembelea hapo kujifunza jinsi ya ujenzi wa masoko hayo ya wamachinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meya ahimiza uzalendo mradi anwani za makazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, amewataka vijana waliopata ajira za muda kutekeleza mradi wa uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi, kufanya kazi kwa uaminifu, uangalifu na uzalendo ili kukamilisha kwa wakati.

Prof. Mwamfupe alitoa rai hiyo juzi jijini Dodoma alipozungumza na vijana 300 walioajiriwa na Halmashauri ya Jiji hilo kwa ajili ya kufanya kazi hiyo kwa siku 45 katika kata 41 na mitaa 222.

Alisema vijana hao wanapaswa kutumia lugha nzuri kwa wananchi pindi watakapokwenda kuifanya kazi hiyo na kuwa mabalozi wa kutoa elimu kwa jamii ili mradi ufikie malengo yake.

Meya alisema halmashauri haitasita kumwondoa kijana yeyote atakayebainika kutaka kukwamisha mradi huo kwa kuharibu kazi aliyopewa. "Tutamchomoa mtu yeyote miongoni mwenu ambaye alipata ajira hii ya muda ya mradi huu wa mfumo uwekaji wa anwani za makazi na postikodi ndani ya mitaa yetu 222, ambaye atabainika kutaka kuharibu na kukwamisha," alionya.

Mratibu wa Mfumo wa Uwekaji wa Anwani za Makazi na Postikodi wa Jiji hilo, Joseph Nkuba, alisema kazi hiyo imepangwa kikamilika Aprili 17, mwaka huu na kuwahimiza vijana hao kuzingatia maelekezo. Vilevile, aliwataka wakazi wa jiji hilo kutoa ushirikiano kwa vijana hao ili kupata taarifa sahihi kwenye maeneo yao.

# Wakazi 6,700 kupatiwa maji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKALA wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) unatarajia kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Chahwa jijini Dodoma kabla ya Juni 30, mwaka huu, ili kuwaondolea adha ya upatikanaji wa maji wakazi 6,747.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwenye maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kwenye Kata ya Chahwa juzi, Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Haidani Ally, alisema gharama za mradi huo ni Sh. milioni 689.7 na unatekelezwa kwa utaratibu wa 'force account'.

"Awali tulipanga kutekeleza mradi kwa kutumia mkandarasi kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) kwa gharama ya Sh. milioni 842.1 lakini baada ya maelekezo kutoka RUWASA Makao Makuu tulipitia upya mradi na gharama za makisio zikawa Sh. milioni 689.7 kwa kutumia 'force account'," alisema.

Alibainisha kuwa shughuli za ujenzi wa mradi zilianza kutekelezwa Aprili 20, 2020 na ulitakiwa kukamilika Juni 30, 2021 lakini kutokana na vikwazo mbalimbali, sasa utakamilika kabla ya Juni 30, mwaka huu na kukabidhiwa kwa wananchi wenyewe.

Alisema kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji huo umeshafanyika ikiwamo ujenzi wa tangi la maji lita 100,000 juu ya mnara wenye urefu wa mita 12, uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa kilometa 2.9 na kulaza bomba kuu kutoka katika kisima hadi kwenye tangi, kujenga nyumba ya mfumo wa kuvuta na kusukuma maji na ufungaji wa mfumo wa umeme jua.

Alisema kazi zingine zilizofanyika kwenye mradi huo ni uchimbaji wa mitaro kwa ajili ya kulaza mabomba ya usambazaji maji wenye urefu wa kilometa 9.8 na uandaji na usajili wa chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO).

Pia ujenzi wa magati ya kuchotea maji 17 pamoja na kufanya usanifu wa mtandao wa maji kwa ajili ya kuwafikishia kwenye mitaa ya Mahoma Makulu, Chibefu na Mpemba–Moto iliyoko kwenye kata hiyo.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwataka wananchi kupanda miti kwa wingi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na kuepuka kuharibu miundombinu.

"Hapa ninaomba nisisitize kwa viongozi wa mitaa iliyoko kwenye kata hii ya Chahwa, iwe wajibu wenu kulinda na kutunza vyanzo vya maji na kusimamia kwenye nafasi zenu ili kudhibiti wale wote wanaoharibu vyanzo hivyo muhimu kwa ajili ya wananchi wa kata hii," aliagiza.



## Mitaro yawa kero kwa wajasiriamali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJASIRIAMALI wanaofanya biashara ya chakula kwenye vibanda vinavyozunguka Kituo cha Mabasi Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuboresha mitaro ya maji ili kuondoa maji ya mvua yanayotuama kwenye maeneo ya biashara zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, wajasiriamali hao walisema kipindi hiki cha mvua wanakosa wateja kutokana na maji kujaa kwenye vibanda vyao na hata kuziba njia zinazoingia kwenye maeneo yao ya biashara.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Sharifa Simbeye, alisema hali hiyo inasababishwa na mitaro iliyoko kuwa midogo na hivyo kushindwa kuhimili wingi wa maji ambayo huwa yanapita kwenye eneo hilo mvua inaponyesha.

Alisema maji hayo wakati mwingine yanakuwa machafu kutokana na kusomba taka kutoka maeneo ya sokoni na barabarani na hivyo kutoa harufu ambayo huwa inawafanya wateja kutoingia kwenye maeneo hayo.

"Tunaiomba serikali itusaidie kwa sababu hizi biashara zetu zinatusaidia kulea watoto na kuendesha maisha yetu kwa ujumla, lakini sisi siyo kwamba hapa tunafanya biashara bure, tunalipa kodi," alisema Sharifa.

Alisema mazingira hayo yanawasababishia kushuka kiuchumi kutokana na kutumia mitaji mikubwa lakini faida hawapati na wakati mwingine wanamwaga vyakula.

Hawa Kajembe, mjasiriamali katika eneo hilo, alisema mara nyingi maofisa afya wamekuwa wakiwasisitiza kufanya biashara ya chakula kwenye mazingira rafiki, lakini mitaro hiyo inawafanya washindwe kuwa safi kama inavyotakiwa.

Alisema kinachotakiwa ni mitaro iliyoko kupanuliwa ili iwe na uwezo wa kuhimili maji ambayo huwa yanapita katika eneo hilo na kutoruhusu maji kusambaa kwenye maeneo ya biashara zao.

Alisema mitaro iliyoko wakati mwingine huwa inaziba kutokana na maji kusomba taka ambazo huzuia maji kwenda kwa kasi na hivyo kuanza kujaa na kuingia kwenye vibanda vya biashara zao.

Alisema kwa sasa biashara yao ni mbaya na wanashindwa hata kufanya shughuli za maendeleo kutokana na faida kuwa ndogo na wakati mwingine hawapati faida.

"Biashara zetu kwenye hili eneo huwa zinakuwa nzuri sana kiangazi kutokana na wateja kuingia bila shida yoyote. Kwa sasa hali ni ngumu sana, mvua ikipungua kuna maji huwa yanatuama humo kwenye mitaro na yananuka," alisema Hawa.

Diwani wa Utengule Usongwe kiliko kituo hicho cha mabasi, Yohana Ntunjilwa, alikiri uwapo wa tatizo hilo na tayari hatua zimeanza kuchukuliwa na serikali kuhakikisha mazingira ya biashara yanakuwa rafiki kwa wananchi.

Alisema kwa sasa serikali imeanza na uboreshaji wa miundombinu ya barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kwa kupanua mitaro na kuchimba mtaro mkubwa unaopeleka maji Mto Mbalizi kutoka katika barabara kuu.

Alisema kuwa baada ya kukamilisha mitaro hiyo, serikali ina mpango wa kuboresha kituo hicho cha mabasi kwa kuboresha mitaro na kutengeneza vizuri baadhi ya miundombinu.

Alisema tatizo lililoko siyo kero kwa wajasiriamali hao pekee, bali hata kwa watumiaji wengine wa kituo hicho wakiwamo madereva ambao wamekuwa wakilalamikia miundombinu ya barabara.

# RC ataka maboresho ya maslahi ya walimu

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu wa ngazi zote pamoja na maofisa elimu ili kuongeza ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa.

Juma Homera alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha wadau wa elimu kilichoitishwa kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali ya sekta hiyo.

Alisema baadhi ya wakurugenzi wamekuwa wakitumia lugha za kuwakatisha tamaa walimu, ikiwamo kuwatupia lawama pale matokeo ya wanafunzi yanapokuwa hayaridhishi ilhali wao wenyewe hawajawajibika kuboreshea mazingira ya kazi.

Homera alisema kuwa wakati mwingine maofisa elimu wamekuwa wakishindwa kwenda kutembelea shule kutokana na kukosa magari na wakati mwingine gari linakuwapo, lakini mafuta wanakosa.

Alisema watumishi hao hawawezi kufanya kazi kwa ufasaha kama maslahi yao yanakwamishwa na wakurugenzi na hivyo akawataka wakurugenzi wenye tabia za aina hiyo kuacha kufanya hivyo.

"Wakati mwingine kama ofisa elimu ni mwanamke, akienda kuomba stahiki zake kwa mkurugenzi ambaye ni mwanamume, atazungushwa mpaka na mambo mengine, hawa watu jamani ni binadamu kama ilivyo kwenu," alionya.

Homera alisema kuwa walimu na maofisa elimu wana majukumu ya kifamilia kama ilivyo kwa watu wengine, hivyo wanatakiwa kutimiziwa mahitaji yao ili wafanye kazi bila kuwa na mawazo ya aina yoyote yanayoweza kukwamisha kazi.

Alisema wakurugenzi wanapowataka walimu walete matokeo mazuri, wanatakiwa kwanza waboreshe maslahi ya walimu ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

Alisema wapo baadhi ya maofisa elimu wana tabia ya kujigeuza miungu watu, wakitaka kuogopwa na walimu huku baadhi yao wakidaiwa kuzuia ruhusa za walimu bila sababu za msingi.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema mkoa huo umekuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanafaulu na kuendelea na masomo ya ngazi ya juu.

Alikumbusha kuwa katika matokeo ya kidato cha nne mwaka jana, mkoa huo ulikuwa miongoni mwa mikoa iliyotoa idadi kubwa ya wanafunzi vinara kwa kutoa wanafunzi saba kati ya 10 waliofanya vizuri.

"Shule yetu ya St. Francis iliongoza kitaifa na ilitoa wanafunzi saba vinara. Sasa niwaombe wadau tuendelee kushirikiana kuboresha sekta hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu," alisema Mwalimu Hinju.

Alisema maendeleo mazuri ya sekta ya elimu yanategemea ushirikiano kati ya walimu, wazazi na wadau wengine wa elimu, akisisitiza sekta binafsi pia ni muhimu katika kuinua sekta ya elimu.



Mgambo wa Jiji la Mbeya wakibeba bidhaa za wajasiriamali wanaodaiwa kufanya biashara zao katika maeneo yasiyoruhusiwa, Kabwe jijini humo jana. Wafanyabiashara hao wanatakiwa kwenda uwanja wa ndege wa zamani walikotengewa kufanya shughuli zao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC Rungwe aonya ukwepaji wa kodi

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya amewaonya wafanyabiashara wa mazao wilayani humo wanaokwepa kulipa ushuru wa mazao na kodi zingine kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Dk. Vincent Anney alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na baadhi ya wafanyabiashara wa maparachichi wilayani humo kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu zao hilo.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakikwepa kulipa tozo za kisheria na kusababisha halmashauri kukosa mapato na hivyo kushindwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa ufasaha.

Aliwataka kuacha mara moja tabia hiyo kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi na endapo watapatikana, watachukuliwa hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

"Hatutaki kuanza kufukuzana na watu lakini ikitubidi tutafanya hivyo. Kuna baadhi wamekuwa wakikwepa kwa makusudi kulipa ushuru, tutaanza kumchukulia mmoja mmoja hatua za kisheria mpaka tukomeshe tabia hiyo," alionya.

Dk. Anney alisema kuwa kwa sasa serikali inaendelea kuwahimiza wananchi wa wilaya hiyo kulima kwa wingi maparachichi kwa kuwa ni miongoni mwa mazao yenye soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Aliwataka kuendelea kuzalisha kwa kutumia mbinu za kisasa, ili kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa pamoja na kuongeza uzalishaji kwa kutumia miche ya kisasa.





Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, akichangia mada katika kikao maalum cha kuwasilisha utiaji wa saini mkataba wa kuziondoa baadhi ya kero za kibiashara kati ya Tanzania na Kenya zilizopatiwa ufumbuzi mjini Zanzibar, mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi ageukia ushirikishaji wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo na kufanya uamuzi ni muhimu kwenye kujenga na kuendeleza utawala bora nchini.

Dk. Mwinyi alihimiza kuhusu suala hilo juzi wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa asasi za kiraia uliofanyika mjini Unguja.

Alisema hatua hiyo ni muhimu kutokana na asasi za kiraia kuwa karibu na jamii na zinatambua matatizo yanayowagusa wananchi.

Alizitaka asasi za kiraia kushirikiana na serikali katika kuimarisha utoaji wa huduma ikiwamo elimu, afya, maji, kupiga vita vitendo vya ufisadi, rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema maendeleo ya nchi hayaletwi na serikali pekee, bali asasi za kiraia nazo zina jukumu hilo.

Rais Dk. Mwinyi aliahidi kufanya kazi kwa ushirikiano na asasi za kiraia katika ujenzi wa taifa huku akizitaka kujikita katika kuimarisha amani, demokrasia na uchumi wa maendeleo ya kijamii na kuacha kufanya kazi kwa malengo binafsi.

Alisema mafanikio ya utulivu wa kisiasa kwa kiasi kikubwa yanatokana na kuwapo kwa asasi za kiraia ambazo zimejikita katika kutoa elimu hiyo kwa makundi ya wananchi nchini.

Alisema pia alieleza kufurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na asasi za kiraia ya The Foundation for Civil Society (FCS) ambayo imekuwa ikitekeleza mradi mkubwa wa kudumisha amani nchini kwa kushirikiana na asasi zingine kufikisha ujumbe wa amani.

"Nachukua nafasi hii kukumbusha majukumu ya asasi za kiraia kuona kwamba zinajikita na kufanya kazi moja kwa moja katika malengo yaliyokusudiwa katika usajili wao na sio kufanya kazi kisirisiri," alionya.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalumu SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema serikali imejipanga kufanya kazi kwa karibu na asasi za kiraia na kuona michango yake katika uchumi wa bluu inawafikia walengwa.

Alisema kwa kuonyesha mfano wa ushirikiano na asasi za kiraia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mkutano wa asasi hizo pamoja na maonyesho yake kwa pamoja yametayarishwa na serikali na mwamvuli wa asasi za kiraia (ZANGOZ).

"Serikali ya Mapinduzi tunafanya kazi kwa pamoja na asasi za kiraia kuona malengo yao yanafikiwa hatua ambayo hata haya maonyesho ya mwaka huu tumeshirikiana nao kwa pamoja," alisema.

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alisema nchi yake inasaidia asasi za kiraia zenye mwelekeo wa kujenga demokrasia na vijana.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya umoja wa kitaifa kwa kazi kuwa ya kuwaunganisha wananchi na kuondokana na siasa za chuki na uhasama.

"Marekani tunaunga mkono maridhiano ya kisiasa yaliyounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Zipo asasi za kiraia tumeziwezesha kutoa elimu katika eneo hilo kuona maridhiano yanajikita katika demokrasia zaidi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwango, alisema Zanzibar kuna asasi za kiraia 96 zimewezeshwa kwa kupewa ruzuku ya Sh. bilioni 4.8 kutekeleza majukumu yao ikiwamo kutoa elimu ya kudumisha amani, demokrasia na haki za binadamu.

Baadhi ya viongozi wa asasi za kiraia walioshiki katika mkutano huo ambao umeambatana na maonyesho, wamefurahishwa na mahudhurio ya mkutano huo ambao watapata nafasi ya kuelezea majukumu ya utendaji wa kazi zao.

# Viwanda vikubwa kujengwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imesema inakusudia kujenga viwanda vikubwa vya uwekezaji ili kuwainua wananchi kiuchumi.

Katika kikao maalumu na wawekezaji kutoka nchi za Kuwai na Uturuki kilichofanyika mjini Unguja jana, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema ujio wa wawekezaji hao ni ishara tosha ya kuonyesha utayari wao katika kuisaidia Zanzibar kiuchumi.

Alisema serikali imetoa vipaumbele kwa baadhi ya maeneo ikiwamo uchumi wa bluu, miundombinu, nishati na viwanda ili kuwawezesha wananchi kujiinua kiuchumi na kuleta maendeleo katika nchi.

Alisema ujio wa wawekezaji utasaidia kuimarisha huduma muhimu ambazo zinapokosekana, zinasababisha ukosefu wa ajira kwa wananchi.

Waziri huyo alisema wawekezaji hao watawekeza katika maeneo yaliyopewa kipaumbele na serikali ikiwamo viwanda vya chakula na nishati ambavyo ni mahitaji muhimu kwa wananchi na kulifanya taifa kujitegemea hasa wakati wa majanga.

Wawekezaji hao walisema wako tayari kushirikiana na Serikali ya Zanzibar kuwekeza hasa kwenye maeneo yaliyopewa kipaumbele na serikali ili kuliongezea Pato la Taifa.

Kikao hicho kiliwashirikisha watendaji wa SMZ wakiwamo mawaziri na manaibu wao pamoja na makatibu wakuu wa wizara zilizopewa vipaumbele, wakijadili mambo mbalimbali ya kimaendeleo nchini.

# ACT-Wazalendo yataka kilimo kikidhi mahitaji utalii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wakulima kuitumia vyema rasilimali ardhi iliyoko kuendeleza shughuli za uzalishaji wa kilimo kinachoendana na mahitaji ya soko la utaalii.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alieleza hilo jana katika mashamba ya ushirika wa wakulima wa ndimu na nyanya huko Bwejuu Mkoa wa Kusini Unguja akiwa katika ziara yake ya kichama mkoani humo.

Alisema kwamba rasilimali ya ardhi iliyoko iwapo itatumika vyema na kwa kuangalia mahitaji ya soko hasa la utalii lililoko nchini, kilimo chao kitakuwa na tija kubwa na kuwasaidia kuongeza kipato kinachotokana na kilimo hicho.

Othman alisema Zanzibar kwa sasa ina zaidi ya hoteli za kitalii 600 zenye mahitaji makubwa ya bidhaa za kilimo, lakini wakulima walioko hawajafikia kiwango cha mahitaji ya soko hilo. Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwasaidia wakulima hao ili kutumia utaalamu na mbinu bora na mbadala ikiwamo teknolojia ya kisasa ya uzalishaji ili kuzalisha kwa viwango na kuongeza tija ya kazi zao.

Katibu wa Ushirika wa Wakulima wa Ndimu na Nyanya, Ali Abdalla Simai, alisema ushirika huo unakabiliwa na uhaba wa nyenzo ikiwamo mtaji wa kuwezesha kununua vifaa vya kuendesha kazi zao.

Alisema kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta ambayo yanatumika kwa ajili ya jenereta ili kumwagilia maji katika mashamba yao na bei ya nyanya kushuka, kunachangia kilimo hicho kutokuwa na tija kwao.

Alisema kuna haja kuwapo mbinu mbadala za uzalishaji kwa kutumia gharama nafuu, akiomba serikali kuharakisha upatikanaji wa huduma za umeme katika eneo hilo ili shughuli zao za umwagiliaji zifanyike kwa wepesi zaidi.

# Ukatili watajwa tishio Morogoro

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUMO wa utafutaji ridhiki na wazazi kutowajibika katika malezi ya watoto kumetajwa kuchangia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto mkoani Morogoro.

Kutokana na ongezeko hilo la vitendo vya ukatili, Kituo cha Mkono kwa Mkono kinachohudumia watoto waliokumbwa na vitendo vya ukatili kilichoko Manispaa ya Morogoro, kimewataka wanawake kuwajibika katika malezi ya watoto ili kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mratibu wa kituo hicho kilichoko chini ya Chuo Kikuu cha Jordan, Virginia Bamulange, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu nafasi ya mwanamke katika kupambana na vitendo vya ukatili mkoani Morogoro.

Bamulange alisema kuwa chanzo cha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni kutowajibika kwa jamii hususani wanawake katika malezi ya watoto na kuwataka sasa wazazi na walezi kuanza kuwajibika.

"Ni muhimu sasa wazazi hasa wanawake kuwajibika katika malezi ya watoto. Ni lazima ufuatilie mwenendo mzima wa mtoto wako kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha. Hii itasaidia kuzuia vitendo vya ukatili kutokea," alisema Bamulange.

Mratibu huyo aliitaka jamii na wazazi kuanza kuzungumza na watoto kuhusina na masuala ya uzazi na vitendo vya ukatili kwa uwazi ili wanapokutana navyo waviepuke au kupambana navyo.

Mganga wa kituo hicho, Dk. Elias Mtungilwa, alisema vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vimekuwa vikichangiwa na wazazi au walezi kukimbizana katika kutafuta ridhiki za kila siku na kukosa muda wa kuwa karibu na watoto kujua matatizo yao.

Dk. Mtungilwa alisema kutokana na mfumo huo wa maisha, sasa kumezuka aina mpya ya ukatili dhidi ya watoto ambayo ni kutelekezwa ukiachana na vitendo vingine vya ukatili kwa watoto ambavyo wamekuwa wakifanyiwa.

Tumaini Kachocho kutoka jamii za kifugaji wilayani Mvomero mkoani Morogoro, alisema bado wanakabiliwa na tatizo la ukatili ikiwamo ndoa za utotoni na mimba za ututoni, hali ambayo imekuwa kikwazo kwa mtoto wa kike kufikia ndoto zake hasa kielimu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, akizungumza na wanawake walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, alikemea vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kutaka jamii kufichua wanaohusika na vitendo hivyo ili wachukuliwe hatua za kisheria.




Mkurugenzi Mtendaji wa TAHA, Dk. Jackline Mkindi, ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Tanzania akimwonyesha mgeni rasmi pamoja na wageni wengine unga uliotengenezwa na zao la ndizi na mmoja wakulima ambao wanasimamiwa na taasisi hiyo, katika banda la TAHA. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waziri aagiza kushushwa vyeo vigogo 23 TAMISEMI

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amemwelekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, kuwashusha vyeo wakuu wa vitengo vya ununuzi na ugavi 23 kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Bashungwa ametoa maelekezo hayo baada ya kufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi kwa baadhi ya wakuu wa idara na vitengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyoelekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa ziara yake mkoani Mara Februari 5, mwaka huu.

"Tathmini iliyofanywa ililenga kupima uhalisia wa utendaji kazi wa wakuu wa idara na vitengo katika utoaji wa huduma na utekelezaji wa shughuli za maendeleo, ujazaji wa nafasi wazi za wakuu wa idara na vitengo, kuboresha na kuondoa changamoto za utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Tathmini ya utendaji kazi wa wakuu wa vitengo vya ununuzi na ugavi imefanyika ili kubaini utendaji kazi wa watumishi hao katika kusimamia masuala mbalimbali ya ununuzi wa umma.

"Baada ya tathmini hii kukamilika katika kitengo cha ununuzi na ugavi, hatua mbalimbali zimechukuliwa zenye lengo la kuimarisha utendaji kazi ambapo Prof. Shemdoe amewashusha vyeo na kuwapangia majukumu mengine wakuu wa vitengo vya ununuzi 23 ambao wamethibitika kuwa utendaji kazi wao haukuwa wa kuridhisha," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Prof. Shemdoe amebainisha kuwa wapo watumishi ambao hatua za kinidhamu na jinai

zinaendelea kuchukuliwa dhidi yao na watachukuliwa hatua stahiki kulingana na matokeo ya kesi zao.

Ilifafanuliwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa Katibu Mkuu amesema kuwa ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, tathmini kama hizo zitaendelea kufanyika kwa watumishi wa kada zingine.

Pia amewaelekeza Makatibu Tawala Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuchukia hatua za kinidhamu kwa watumishi wote wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma kwenye maeneo yao.

# Bolt Tanzania yaja na chaguo bei kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya usafirishaji ya Bolt imesema itawapa wateja wake chaguo la bei, ili kuhakikisha Watanzania wananufaika na huduma hizo.

Kampuni hiyo inakuja na njia kadhaa kwa wadau wake, wakiwamo wafanyabiashara wakubwa na wa kati, kwa lengo la kutoa huduma kwa Watanzania katika nyanja mbalimbali na kutimiza mahitaji ya usafiri.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, kampuni hiyo imekuja na huduma ya Bolt Business inayohudumia wafanyabiashara wadogo, wa kati na kampuni kubwa mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Arusha kwa bei ya makubaliano.

"Bolt Business ni huduma ya kuaminika na imekuwa ikifanyika kwa wakati unaotakiwa, wateja wanaotumia usafiri huu wanaweza kuagiza huduma hii kwa njia ya mtandao na huduma hizo kuwafikia mahala waliko pasipo kuchelewa," alisema Meneja Mauzo wa Bolt Business nchini, Milu Kipimo.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa kupitia mfumo wa Bolt Business, kampuni zinafungua akaunti na kwamba makundi mbalimbali yanaweza kuomba usafiri kwa madereva, pia kufuatilia njia na gharama za safari za biashara na kampuni.

"Biashara ya Bolt inalenga kusaidia kampuni kusimamia vyema safari zao za biashara. Kupitia huduma hiyo, wafanyabiashara hupata udhibiti wa mahitaji yao ya usafiri na usafiri kupitia matumizi ya utaratibu huu.

"Tumejitolea kuwapa wateja wetu urahisi wa kuchagua mfumo wa usafiri wanaoutaka kwa kuzingatia bei," alisema.


Aliongeza kuwa biashara ya Bolt inakuza dhamira ya utoaji wa huduma bora kwa kuwa hurahisisha usimamizi wa usafirishaji wa wafanyakazi wa kampuni mbalimbali kutoka eneo moja hadi lingine.

"Huduma hii inaruhusu ufuatiliaji wa matumizi ya kampuni, inaruhusu chaguo la uhifadhi wa gari, na njia za malipo zilizoboreshwa huku zikitoa uwazi kupitia ripoti za kila mwezi na kutoa fursa kwa wateja kufurahia huduma bora," alihitimisha.

HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA DHIDI YA UKRAINE

# ‘NATO haitaijibu Russia ndani ya Ukraine, kuepusha vita vya tatu vya dunia’



Vita na matumaini. Wanamuziki wa bendi ya Kyiv-Classic Symphony Orchestra wakitoa burudani eneo la Independence Square, mjini Kyiv, nchini Ukraine, mwishoni mwa wiki. **PICHA: AFP**

**Kyiv,** UKRAINE

KWA mara ya kwanza Rais wa Marekani, Joe Biden, ameelezea sababu ya Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi (NATO), kujiepusha na kuingia kijeshi kwenye ardhi ya Ukraine, dhidi ya Russia, akisema makabiliano ya moja kwa moja yatasababisha vita vya tatu vya dunia (WWIII).

Biden amekataa mara kwa mara kutuma wanajeshi wa Marekani dhidi ya Russia nchini Ukraine na badala yake utawala wake umeendesha kampeni ya vikwazo dhidi ya Vladimir Putin na nchi yake.

Mwishoni mwa wiki, Biden alitangaza kupiga marufuku uagizaji wa vodka ya Kirussia, almasi na dagaa.

Rais Biden, pia alidokeza kuwa atazuia mauzo ya nje ya bidhaa za anasa za Marekani, sekta ambayo inazalisha Dola za Kimarekani milioni 550 kwa mwaka.

Miongoni mwa bidhaa ambazo soko la Russia, halitaweza kupata ni saa, magari na vito vya mapambo.

Marekani na washirika wake wanadaiwa kutafuta kubatilisha hadhi ya Russia kama mshirika wa kudumu wa kibiashara, mojawapo ya kanuni za kimsingi za biashara ya kimataifa ambazo Shirika la Biashara Duniani linaziangalia.

“Putin ni lazima alipe gharama,” Rais Biden anasema.

Umoja wa Ulaya (EU), G7 na washirika wa NATO pia wanatarajiwa kujiunga.

Ingawa Biden anahitaji kungwa mkono na Bunge la Marekani, haitarajiwi kwamba atakuwa na matatizo katika kutekeleza hatua hiyo, kwa vile anaungwa mkono na wajumbe wa Chama cha Democratic na Republican katika masuala yanayohusiana na mzozo kati ya Ukraine na Urusi.

> Vikosi vya Russia bado vinajaribu kuuzingira mji wa Kyiv. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky ameahidi kukabiliana na mashambulizi yoyote dhidi ya mji huo.

### SIKU 19 ZA MASHAMBULIZI

Ijumaa, iliporipotiwa kwamba jeshi linaloongozwa na Moscow lilizidisha mashambulizi yake kuelekea Magharibi mwa ardhi ya Ukraine, kwa mashambulizi ya mabomu katika Lutsk na Ivano-Frankivsk, miji karibu na Poland na Moldova. Poland ni mwanachama wa NATO.

Kambi ya kijeshi huko magharibi, karibu na mpaka wa Poland, imeshambuliwa jana Jumapili asubuhi.

Mashambulizi hayo, ambayo yamelenga kituo cha mafunzo ya kijeshi cha Yavoriv, yamesababisha vifo vya makumi ya watu.

Vikosi vya Russia bado vinajaribu kuuzingira mji wa Kyiv. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky ameahidi kukabiliana na mashambulizi yoyote dhidi ya mji huo.

Kusini mwa nchi, shambulio la bomu limeua watu kadhaa huko Mykolaiv mapema Jumapili, hatua ya mwisho kabla ya bandari ya Odessa.


Mji wa Mariupol, ambao bado umezingirwa, ulikuwa unajiandaa siku ya Jumamosi kupokea msafara wa msaada wa kibinadamu ambao ulikuwa umezuiliwa kwa zaidi ya miaka mitano katika kituo cha ukaguzi cha vikosi vya Russia.

Kwa upande wa kidiplomasia, Emmanuel Macron na Olaf Scholz walizungumza na Vladimir Putin siku moja baada ya mkutano wa kilele wa Versailles.

Wito wao wa kusitishwa kwa mapigano haujasikilizwa, huku Rais wa Russia akishutumu vikosi vya Ukraine kwa ukiukaji wa wazi wa sheria za kibinadamu.



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky



Rais wa Marekani, Joe Biden.

Rais wa Ukraine amebaini kuwa takriban wanajeshi 1,300 wa Ukraine wamefariki tangu kuanza kwa mashambulizi ya Russia. Kufikia sasa watu 2,698,280 wameitoroka Ukraine, kufuatia uvamizi wa Russia, kulingana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR).

Idadi ya raia wanaoukimbia mji wa Kyiv imeongezeka wakihofia ukaribu wa jeshi la Russia umbali wa kilomita 25 kutoka mji mkuu huo.

Meya wa Mariupol anasema shambulio dhidi ya mji huo siku 12 zilizopita uliua mamia ya watu.

Marekani imesema itapeleka silaha na vipingamizi mabomu nchini Ukraine yenye thamani ya Dola za kimarekani milioni 200, huku Russia ikidai itashambulia maeneo yenye silaha zitokazo Magharibi.

Ongezeko la bei ya vyakula Afrika Kaskazini kuelekea Ramadhani.

Familia nyingi huko Afrika Kaskazini zinapambana kuhifadhi unga na vyakula vingine muhimu wakati bei ya vyakula ikipanda baada ya uvamizi wa Russia nchini Ukraine, ambao ni wauzaji wakuu wa ngano katika eneo hilo.

Changamoto hiyo inakuja wiki chache kabla ya kuanza kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Waislamu hufunga alfajiri hadi jioni.

Tunisia, Morocco na Libya, sambamba na mataifa kadhaa ya Kiarabu hutegemea kwa kiasi kikubwa ngano ya kutoka Ukraine na Russia.

Wengine wanahofia uvamizi wa Russia unaweza kusababisha njaa na machafuko, huku wakikumbuka jinsi ya kupanda kwa bei ya vyakula kulivyochangia katika vuguvugu la uasi katika nchi za Kiarabu muongo mmoja uliopita.

Bei ya vyakula ilikuwa tayari imeongezeka katika eneo la Afrika Kaskazini hata kabla ya Urusi kuivamia Ukraine zaidi ya wiki mbili zilizopita.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# MCHENGERWA NA VITUO VYA MICHEZO DAR, TANGA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, amesema kukamilika kwa vituo viwili vya michezo vinavyojengwa katika Mkoa wa Tanga na Dar es Salaam, ni mwanzo mzuri wa kuzalisha timu bora za taifa kwenye mchezo wa soka.

**Mchengerwa alitoa kauli hiyo wiki iliyopita wakati alipotembelea mradi wa Kituo cha Michezo kinachojengwa katika eneo la Kisarawe Two, Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam.**

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho na kile kinachojengwa jijini Tanga kutasaidia kutoa hifadhi ya mafunzo katika mpango kabambe wa kuendeleza vipaji vya michezo nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa ambao unatarajiwa kuanza kutekelezwa kupitia wizara yake.

"Ni lazima tukiri kwamba anguko la mchezo wa soka hapa nchini linachangiwa na kiwango kikubwa na miundombinu hafifu ya michezo, kwa hiyo uwapo wa viwanja hivi vyenye sifa za kimataifa, utasaidia kukuza vipaji vya michezo hasa katika mpango wetu wa wizara wa kuibua vipaji nyumba kwa nyumba na mtaa kwa mtaa," alisema Waziri Mchengerwa.

Alisema kukamilika kwa mradi huo pia kutaisaidia serikali kufanya usimamizi dhabiti wa mchezo wa soka, pamoja na kupata mawakala wazuri wenye uwezo wa kusimamia vipaji vya watoto na kuwatafutia fursa ya kucheza soka nje ya nchi kama sehemu ya kuitangaza Tanzania na kuongeza ushawishi kwa vijana kutumia vipaji vyao kwa faida.

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema ujenzi wa kituo hicho cha michezo cha Kigamboni unagharimu dola bilioni mbili na elfu 78 na mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, mwaka huu.

Naye Mkurugenzi wa Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema pamoja na ujenzi wa vituo hivyo viwili vya michezo, Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo tayari ipo kwenye hatua za mwisho kabisa za kuvifanyia ukarabati mkubwa viwanja vya michezo katika shule teule 56 pamoja na kuboresha miundombinu katika kituo cha michezo cha maendeleo ya michezo cha Malya.

## *Shindano la kusaka 'dansi' wa taifa laanza Dar*

**Na Mwandishi Wetu**

SHINDANO la Sanaa ya Kucheza Muziki wa Dansi, kutafuta washiriki wa Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa ya mwaka 2024, limeanza jana jijini Dar es Salaam likiwa na lengo la kusaka vijana 30 watakaoshiriki kinyang'anyiro hicho cha kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa shindano la awamu ya pili lililofanyika kwenye Kituo cha Utamaduni na Sanaa cha Kukaye Moto, Mratibu wa shindano hilo, Ramadhan Mohamed, alisema linashirikisha vijana wakike na wakiume kutoka katika mikoa mbalimbali ambapo mpaka sasa wamepata washiriki kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Kigoma.

Alisema katika kuendesha shindano hilo, wamepata baraka zote kutoka Baraza la Taifa la Sanaa (BASATA).

"Mashindano haya ya kimataifa yatafanyika mwaka 2024, tunaanza mapema kusaka washiriki ili kupata muda wa kujiandaa zaidi kimbinu na kifedha kuweza kushiriki kwa ufasaha zaidi," alisema Mohamed. Mohamed pia aliiomba serikali kupitia kwa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kuwasaidia kufanikisha malengo yao.

"Mpaka sasa tayari tumepata washiriki 10, wakike watano na wakiume watano, tunaendelea kuwatafuta wengine 20 kutimiza idadi ya vijana wachezaji 30," alisema Mohamed.

Mmoja wa washiriki wa shindano hilo kutoka Dar es Salaam, Stephano Mlelwa alisema ameamua kushiriki ili kusaka nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye mashindano hayo kimataifa.




Hassan Mwaterema akipongezwa na wachezaji wenzake wa Kagera Sugar baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikiilaza Mbeya City 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Namungo yaota kubeba ubingwa

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema wao ndio watakaokuwa mabingwa mwisho wa msimu hata kama watu hawawapi nafasi.

Julio amesema kila mechi ambayo wanakwenda kuicheza kwa sasa itakuwa ni kama fainali, kwa sababu wanahitaji kupata alama tatu ambazo zitawafanya wawe mabingwa mwisho wa msimu.

Namungo wanakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi, wakiwa na pointi 25, ambazo ni 20 nyuma ya vinara Yanga wenye pointi 45.

Akizungumza na gazeti hili, Julio aliweka bayana mipango yao ya kutaka ubingwa kwa kuwa wamekuwa na mkakati madhubuti ya kuona lengo hilo linatimia kwa kuwa uwezo wa kufanya hivyo na nia wanayo.

"Namungo tunautaka ubingwa na tutaupata msimu huu, nimekuwa nikiwaambia watu kuhusu hiki mara kwa mara. Uwezo wa kufanya hivyo tunao kwa sababu ndiyo malengo tuliyojiwekea tangu tuchukue timu hii," alisema Julio.

## Tambwe: DTB itacheza Ligi Kuu

**Na Dennis Fussi**

KINARA wa mabao wa Klabu ya DTB inayoshiriki Ligi ya Championship, Amiss Tambwe, amezitaka timu za Ligi Kuu kujiandaa kumdhibiti msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili, mshambuliaji huyo aliyewahi kutamba Simba na Yanga hadi kuibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu, amesema pamoja na ushindani ulioko kwenye ligi hiyo lakini bado ana uwezo wa kuzitikisa nyavu za timu zote kutokana na ubora wa kikosi chao.

"Wajiandae kuzungukwa na moto wa DTB msimu ujao, nataka kufunga kila mechi na uwezo huo ninao bado sijaona timu yenye mabeki wa kunidhibiti," alijigamba Tambwe.

DTB inaongoza ligi ya Championship na inapewa nafasi kubwa kucheza ligi msimu ujao kutokana na ubora wa kikosi cha klabu hiyo ikilinganishwa na timu nyingine.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### LUKAKU KURUDI INTER

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, yuko tayari kukatwa mshahara kwa ajili ya mchakato wa kurejea Inter Milan kwa mkopo. ***(Calciomercato)***

#### JUVE KUNUNUA WAWILI

JUVENTUS wanalenga kuwanunua wachezaji wawili wa kimataifa wa Italia wa Chelsea - kiungo Jorginho mwenye miaka 30 na beki wa kushoto Emerson Palmieri mwenye miaka 27, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Lyon. ***(Tuttosport)***

#### POGBA KUONDOKA UNITED

PAUL Pogba mwenye umri wa miaka 28, ataondoka Manchester United mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Calciomercato)***

#### BARCA KWA ALONSO

BARCELONA pia wanaifuatilia Chelsea na wanavutiwa na wachezaji wao wawili wa kimataifa wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31 na mlinzi wa kulia Cesar Azpilicueta mwenye miaka 32, ambaye mkataba wake unamalizika msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

#### SAUDIA YAITAKA CHELSEA

OMBI la Saudi Media la kutaka kuinunua Chelsea ni pamoja na mipango ya kuunda upya Stamford Bridge na kuwaongezea mikataba wachezaji kama vile Cesar Azpilicueta na mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye miaka 29, ambaye mkataba wake wa sasa unatarajiwa kuisha msimu huu wa majira ya joto. ***(Goal)***

#### SALAH KUBAKI EPL

MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, anataka kusalia kwenye Ligi Kuu England ikiwa hatakubali kusaini mkataba mpya na Liverpool. ***(Football Insider)***

#### ISAK KUTUA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua mshambuliaji wa Real Sociedad, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22. ***(Star)***

#### NIGUEZ ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA watamsajili kiungo wa kati wa Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 27, kutoka Atletico Madrid msimu huu - ikiwa vikwazo vya serikali ya Uingereza vitawaruhusu. ***(Mirror)***


#### LONGSTAFF KUONGEZEWA

KLABU ya Newcastle ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Sean Longstaff, kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto. ***(Times)***

#### JOHNSTONE KUREJESHWA

MANCHESTER United wanaweza kuchukua hatua ya kumrejesha Sam Johnstone kutoka West Brom msimu wa majira ya joto, ingawa Tottenham na Southampton pia wana nia ya kumsajili mlinda mlango huyo wa England mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO: HAKUNA WA KUIZUIA MAN UNITED

**Tumethibitisha tunaweza kuifunga timu yoyote, hakuna mipaka United, twendeni, Mashetani...**

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amesema "hakuna kikomo" kwa Manchester United baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' na kuwaongoza 'Mashetani Wekundu' hao kushinda mabao 3-2 dhidi ya Tottenham Hotspur, Jumamosi.

**Mabao hayo ya Ronaldo kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu England yaliongeza matumaini ya United kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya**

Ronaldo alifunga 'hat-trick' hiyo baada ya miaka 14 na siku 59 kwenye ligi hiyo, kwa mara mwisho alifunga mabao matatu katika ushindi wa 6-0 dhidi ya Newcastle United, likiwa ni pengo refu zaidi kati ya hat-trick ya kwanza na ya pili kwa mchezaji.

Baada ya hat-trick yake ya 49 katika maisha yake ya soka, gwiji huyo wa Ureno pia amefunga mara tatu katika kila msimu kati ya misimu 13 iliyopita ya maisha yake ya klabu.

Ushindi huo wa pale Old Trafford uliipandisha United katika nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu ingawa wamecheza mechi nne zaidi ya Arsenal walio katika nafasi ya tano, na Ronaldo alisema "amefurahishwa sana" na uchezaji wake akiandika kupitia kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

"Nimefurahia sana hat-trick yangu ya kwanza tangu niliporudi Old Trafford," aliandika Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kupitia Instagram yake. "Hakuna kitu kinachozidi hisia za kurejea uwanjani na kusaidia timu kwa mabao na bidii.

"Tumethibitisha kwa mara nyingine kwamba tunaweza kuifunga timu yoyote kwa siku fulani, mradi tu tutafanya kazi kwa bidii na kusimama pamoja kama kitu kimoja.

"Hakuna mipaka kwa Man United! Hata iweje! Twendeni, Mashetani!"

Licha ya matatizo ya United msimu huu, nyota huyo wa zamani wa Real Madrid na Juventus amefunga mabao 12 kwenye ligi tangu arejee klabuni hapo majira ya joto yaliyopita na hivyo kumfanya awe kinara wa ufungaji bora.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

CRYSTAL PALACE
VERSUS
MANCHESTER CITY

1 | 8.29
X | 4.79
2 | 1.37

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ABRAMOVICH AVULIWA UKURUGENZI CHELSEA



**LONDON,** England

LIGI Kuu England imemwondoa mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich kuwa mkurugenzi wa klabu hiyo.

Kamati ya Ligi hiyo imechukua hatua hiyo kumwondoa kutoka katika klabu hiyo baada ya uamuzi wa Serikali ya Uingereza kumwekea tajiri huyo vikwazo kama njia ya kuijibu Urusi kwa kuivamia Ukraine.

Kwa sasa Chelsea imepatiwa kibali maalum cha kuhudumu na kuendelea na shughuli za mpira hata baada ya mali ya Abramovich kuzuiwa na Serikali ya Uingereza.

Ligi Kuu imesema ingawa Abramovich amepigwa marufuku, lakini hatua hiyo "haitaathiri Chelsea kufanya mazoezi na kucheza mpira".

Bilionea huyo amekuwa akiiongoza klabu hiyo tangu mwaka 2003, lakini majaribio yake ya kutaka kuiuza klabu hiyo yalisitishwa na Serikali ya Uingereza, ambayo imezuia mali yake.

Abramovich aliwekewa vikwazo na Serikali ya Uingereza Alhamisi iliyopita kama sehemu ya majibu yake kwa uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine.

Serikali inaamini kuwa bilionea huyo amekuwa na "uhusiano wa karibu kwa miongo kadhaa" na Rais wa Urusi, Vladimir Putin, na Abramovich amekuwa akikanusha mara kwa mara.



## 'Liver ipo tayari kwa ubingwa'

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amebainisha kwamba, wachezaji wa Liverpool wapo tayari kwa mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City katika mechi 10 zilizobaki.

Baada ya mechi 28 kati ya 38 za msimu, zimekuwa ni mbio za farasi wawili kuelekea kwenye ubingwa wa Ligi Kuu, huku City wakiwa na pointi 69 na Liverpool wakiwa na alama 66 baada ya ushindi wa Jumamosi wa mabao 2-0 dhidi ya Brighton.

Timu hizo zimekuwa zikikimbizana kwenye ubingwa wa ligi hiyo tangu msimu wa 2018-19 wakati City walipotwaa ubingwa wakiwa na pointi 98, moja zaidi ya Liverpool ambao walipoteza mchezo mmoja tu.

Alipoulizwa kuhusu mbio hizo, Klopp aliiambia BT Sport: "Hatuwezi kuepuka hilo."

Anajua namna ilivyo ngumu kuikabili City, lakini licha ya pengo lililoko anaamini Liverpool wana nafasi kwenye mbio hizo.

Liverpool watasafiri kwenda kwenye dimba la Etihad kuwavaa Man City mwezi ujao kwenye ligi hiyo.

"Unawatarajia wao kushinda mechi wakati unapowaona wanapocheza," alisema Klopp.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI
CHEZA
SHINDA

# SPORTPESA YAZINDUA HUDUMA YA BET SPINNER

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya SportPesa imetambulisha kwa Watanzania huduma yake mpya ya Bet Spinner, ambayo tayari imezinduliwa rasmi na kuanza kufanya kazi.

**Hii ni huduma inayomwongezea mteja nafasi ya kushinda mara nyingi zaidi ya dau lake analoliweka pindi tu anapoweka ubashiri wake.**

Huduma hii ni moja ya mlolongo wa maboresho na ubunifu katika biddhaa za SportPesa ambapo kwa wiki iliyopita ilishatambulisha Promosheni ya Bet Bonanza kwa ushirikiano wa Vodacom, Airtel pamoja na Halotel.

Akizungumza kuhusu Bet Spinner, Meneja Uhusiano SportPesa, Sabrina Msuya, alisema huduma hii ni maalum kwa wateja wao wenye lengo la kuwaongezea ushindi baada ya kuweka ubashiri wao.

Alisema promosheni hiyo ya Bet Bonanza inawapa Watanzania fursa ya kushinda shilingi 20,000 kila siku, milioni moja kwa wiki na Sh. 5,888,000.

Sabrina alisema tayari washindi zaidi ya 200 kutoka pande zote za Tanzania wamejishindia pesa zao na wengine wakitarajiwa kuendelea kushinda mamilioni kila siku.

"Wateja wetu wanaweza kujishindia mara dufu ya dau lao, mfano umebashiri mechi tano ambazo kiwango cha malipo tarajiwa ni Sh. 50,000, basi Bet Spinner itakuongezea fursa ya kukipandisha kiwango hicho kuanzia mara mbili hadi mara mia moja zaidi ya dau lako.

"Chukulia hiyo 50,000 tarajiwa halafu Bet Spinner ikikupa turufu ya mara sita, basi kiwango chako cha malipo tarajiwa kitapanda mpaka laki tatu," alisema Sabrina.

Sabrina alihitimisha kwa kuwaasa Watanzania kuendelea kucheza kila siku ili kujishindia fedha katika Bet Bonanza na pia kutumia fursa ya Bet Spinner ambayo ni kubwa kabisa kuliko zote na kuendelea kucheza SportPesa Jackpot ambayo kwa sasa imesimamia juu ya Sh. bilioni moja.

Alisema ili kujisajili mteja anatakiwa kupiga *150*87# au kutembelea www.sportesa.co.tz




Meneja Uhusiano na Mawasiliano SportPesa Tanzania, Sabrina Msuya, akizungumza na vyombo vya habari wakati wa uzinduzi wa huduma ya Bet Spinner ikiwa ni mwendelezo wa kuwaongezea wateja wao wigo wa kucheza ili kujiongezea ushindi. **PICHA: SPORTPESA**

# *Msimu akiri msimu mgumu Ligi Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kuwafumua Maafande wa JKU kwa mabao 3-1 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar, timu ya Mabaharia wa KMKM, imekiri umekuwa msimu mgumu na ushindi huo walioupata katika Uwanja wa Amaan juzi, ulikuwa wa jasho haswa.

Katika mechi hiyo iliyopigwa majira ya saa moja usiku, mabao ya KMKM yalipachikwa nyavuni kupitia kwa Adam Ibrahim dakika ya 23', Salum Akida (dk. 81) na Optatus Lupekenya (dk. 90), huku lile la kufutia machozi kwa JKU likiwekwa kimiani dakika ya 73 na Abdulkarim Yunus.

Kwa matokeo hayo, KMKM imefikisha alama 51 zilizotokana na michezo 22 huku ikiwa imebakiza mechi nane kabla ya kuhitimisha msimu huu, wakati wapinzani wao JKU wakisalia nafasi ya pili na pointi zao 41.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema licha ya kutoka na ushindi huo mnene haikuwa rahisi kwani mechi ilikuwa ngumu kwa dakika zote.

Alisema timu zote zilikuwa bora na wachezaji wa vikosi vyote walicheza kwa ushindani mkubwa ili kupata alama tatu.

"Wachezaji walijutuma kwa jasho katika dakika zote za mchezo, mchezo ulikuwa ni wakushambuliana kwa zamu, kipindi cha kwanza tulikiweza, lakini cha pili tulirudisha kasi katika dakika za mwishoni na tukafanikiwa kupata mabao mawili yaliyotupa ushindi mnono wa 3-1," alisema.

Kwa upande wa Kocha wa JKU, Sheha Moh'med, alisema alikipanga kikosi cha ushindi na chenye kutoa matokeo, lakini bahati haikuwa yao.

Alisema baada ya kupoteza mchezo huo sasa anajiandaa na mchezo wa mzunguko wa 23 ili aweze kufuta makosa aliyoyaona katika mchezo huu.

Matokeo mengine katika mzunguko huu wa 22, Mafande wa Mafunzo wamefanikiwa kutoka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mlandege mchezo uliopigwa katika Dimba la Amaan saa tisa Alasiri

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 14/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1153 | Gorilla FC vs Musanze | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 16:00 | 1856 | Basaksehir vs Antalyaspor | 1.74 | 3.53 | 4.61 |
| 16:00 | 2081 | AS Kigali vs Gicumbi | 1.41 | 4.40 | 8.00 |
| 16:00 | 2246 | Novi Pazar vs Mladost Lucani | 2.15 | 3.28 | 3.04 |
| 16:30 | 4931 | Barito Putera vs Persebaya Surabaya | 4.53 | 3.08 | 1.80 |
| 17:00 | 5159 | Adanaspor vs Eyupspor | 3.05 | 3.35 | 2.30 |
| 17:55 | 2937 | Metalac vs Red Star Belgrade | 9.64 | 5.78 | 1.21 |
| 19:00 | 3625 | Rubin Kazan vs Rostov | 1.88 | 3.48 | 3.82 |
| 19:00 | 4561 | Botosani vs Gaz Metan Medias | 1.03 | 11.79 | 39.29 |
| 19:30 | 1184 | Olimpija Ljubljana vs NK Celje | 1.70 | 3.70 | 4.13 |
| 20:00 | 1555 | Rakow Czestochowa vs Stal Mielec | 1.29 | 4.84 | 8.52 |
| 20:00 | 1738 | Bnei Yehuda vs Ironi Hasharon | 2.00 | 3.08 | 4.08 |
| 20:00 | 2935 | Beitar Tel Aviv Ramla vs Hapoel Ramat Gan | 2.86 | 2.91 | 2.66 |
| 20:00 | 3564 | GKS Katowice vs Chrobry Glogow | 2.22 | 3.23 | 2.94 |
| 20:00 | 4531 | AS Ashdod vs El Fahem | 2.82 | 2.82 | 2.77 |
| 20:00 | 5373 | Galatasaray vs Besiktas | 2.45 | 3.29 | 2.75 |
| 20:00 | 5491 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.29 | 3.26 | 3.01 |
| 20:00 | 5843 | Paeek vs Ethnikos Achnas | 2.87 | 3.27 | 2.41 |
| 20:45 | 2237 | Chateauroux vs Laval | 2.21 | 3.09 | 3.23 |
| 21:00 | 1649 | Odense vs Aalborg | 2.28 | 3.30 | 3.01 |
| 21:00 | 2203 | Meppen vs Duisburg | 2.26 | 3.43 | 2.89 |
| 21:00 | 5588 | Malmo vs AIK Football | 1.69 | 3.53 | 4.44 |
| 21:30 | 4466 | Beitar Jerusalem vs Maccabi Haifa | 8.70 | 4.83 | 1.29 |
| 22:00 | 1520 | Den Bosch vs Jong PSV | 2.74 | 3.42 | 2.34 |
| 22:00 | 2265 | Helmond Sport vs VVV Venlo | 3.08 | 3.42 | 2.14 |
| 22:00 | 2588 | Roda Kerkrade vs De Graafschap | 2.27 | 3.37 | 2.88 |
| 22:00 | 2622 | Dordrecht vs FC Oss | 2.79 | 3.42 | 2.31 |
| 22:00 | 3681 | Haladas vs Budafoki Mte | 1.52 | 3.65 | 5.96 |
| 22:00 | 3941 | Telstar vs NAC Breda | 2.83 | 3.37 | 2.30 |
| 22:00 | 4010 | Steaua Bucuresti vs Farul Constanta | 1.72 | 3.48 | 4.70 |
| 22:00 | 4322 | FC Eindhoven vs ADO Den Haag | 1.97 | 3.61 | 3.32 |
| 22:00 | 4912 | Maastricht vs Jong AZ Alkmaar | 2.89 | 3.52 | 2.20 |
| 22:00 | 5367 | Emmen vs FC Volendam | 1.94 | 3.61 | 3.41 |
| 22:30 | 1301 | Leixoes vs Vilafranquense | 1.77 | 3.42 | 4.40 |
| 22:45 | 2043 | Bohemians FC vs Shelbourne | 1.80 | 3.37 | 4.04 |
| 22:45 | 2079 | Dundalk FC vs Shamrock Rovers | 3.04 | 3.23 | 2.17 |
| 22:45 | 2110 | Dundee Utd vs Celtic | 9.63 | 5.59 | 1.22 |
| 22:45 | 3040 | Athlone Town vs Cobh Ramblers | 1.79 | 3.67 | 3.72 |
| 22:45 | 4108 | Sligo Rovers vs Finn Harps | 1.75 | 3.36 | 4.33 |
| 22:45 | 4695 | Cork City vs Waterford Utd | 3.37 | 3.42 | 1.96 |
| 22:45 | 4885 | St Patricks vs UCD Dublin | 1.30 | 4.73 | 8.30 |
| 22:45 | 4969 | Derry City vs Drogheda Utd | 1.50 | 3.86 | 5.79 |
| 22:45 | 5007 | Galway United vs Treaty United | 1.33 | 4.53 | 7.90 |
| 22:45 | 5276 | Lazio vs Venezia | 1.33 | 5.38 | 8.37 |
| 22:45 | 5600 | Longford Town vs Bray Wanderers | 2.23 | 3.17 | 2.98 |
| 23:00 | 2386 | Feralpisalo vs Triestina | 2.19 | 3.15 | 3.50 |
| 23:00 | 2671 | Mallorca vs Real Madrid | 5.34 | 4.09 | 1.59 |
| 23:00 | 3940 | Crystal Palace vs Manchester City | 8.29 | 4.79 | 1.37 |
| 23:00 | 4919 | Llaneros FC vs Fortaleza (COL) | 1.97 | 3.17 | 3.61 |
| 23:15 | 5100 | Moreirense vs Sporting Lisbon | 7.10 | 4.44 | 1.41 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Machi 14, 2022
Nipashe



Ronaldo: Hakuna wa kuizuia Man Utd UKURASA 21

WAMEKAA...



Winga wa Simba, Pape Sakho, akishangilia sambamba na Shomari Kapombe (kulia), baada ya kufungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Aucho, Ushindi wamtuliza Nabi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kurejea kwa baadhi ya nyota wake uwanjani kutoka chumba cha majeruhi, kumepunguza presha kubwa kuelekea katika michezo yao ijayo ya mzunguko huu wa pili wa Ligi Kuu, ambao ameeleza unaushindani mkubwa.

Nyota ambao wamerejea kikosini Yanga ni Abdallah Shaibu 'Ninja', Khalid Aucho, Farid Mussa na Chico Ushindi, jambo ambalo kwake ameeleza ni faraja kubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema baada ya mazoezi ya juzi waliporejea kambini, ripoti ya madaktari inaonyesha wachezaji wasiopungua wanne wamerejea kazini na kufanya mazoezi.

Alisema kurejea kwa nyota hao ni nafuu na ana imani wengine watarejea na mambo yatakuwa mazuri ndani ya kikosi chake, kinachopambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo iliyobaki ya mzunguko wa pili.

"Ni jambo zuri kwetu kuona wachezaji waliokuwa majeruhi wanarejea, nina matarajio makubwa ya kuwa na kikosi imara hasa kwa kipindi hiki cha ushindani mkubwa wa ligi," alisema Nabi.

Kuhusu maandalizi ya kikosi chake kuelekea mchezo wao dhidi ya KMC FC, alisema yanaendelea vizuri na ana matarajio makubwa nyota walitoka katika chumba cha majeruhi watakuwa sehemu ya programu ya mchezo huo.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, kurejea kwa nyota hao kunafanya kikosi kuwa kipana na kupata nafasi ya wachezaji wengine kutumika, nina imani watarejea katika ubora wao na kusaidia timu kufikia malengo yanayotarajiwa," alisema Nabi.

# Simba yafanya yake CAF

## ●●● Sakho aiongoza kuivutisha Berkane 'pumzi ya moto' kwa Mkapa, yakaa kileleni Kundi D, huku...

**Na Adam Fungamwango**

MSENEGAL Pape Sakho, jana alifunga bao pekee lililoipa ushindi Simba ikiichapa RS Berkane ya Morocco bao 1-0 kwenye mechi ya hatua za makundi, Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

**Alipata mpira pembeni kwenye winga ya kushoto kutoka kwa Mohamed Hussein, akaingia nao ndani ya eneo la hatari na kisha kumpasia Meddie Kagere aliyemrejeshea kisha akatishia kupiga akiwahadaa mabeki wa Berkane mara mbili na ya tatu akafumua shuti la chini chini lililojaa wavuni, kushoto mwa kipa Hamza Hamiani, ikiwa ni dakika moja kabla ya kuelekea mapumziko.**

Ni ushindi ambao umeifanya Simba kulipa kisasi cha kufungwa mabao 2-0 Februari 27, mwaka huu, ikiwa ugenini, nchini Morocco.

Haikuwa mechi rahisi kwa Simba, lakini kama wachezaji wake wangekuwa makini, basi wangeweza kuondoka na ushindi zaidi ya huo walioupata.

Dakika ya tatu tu ya mchezo, Simba walilisabahi lango ya RS Berkane baada ya Joash Onyango kuruka juu na kuunganisha kwa kichwa mpira wa kona iliyochongwa na Rally Bwalya, lakini ulitoka sentimeta chache ya lango.

Mwanzoni, Berkane walionekana kulinda zaidi na wakitega mashambulizi ya kushtukiza huku Simba ikionekana kushindwa kuifungua kirahisi na kuishia kucheza mpira katikati mwa uwanja, mashambulizi yao hayakuwa makali, hadi dakika ya 24 Sakho alipoamua kukokota mpira kwa umbali mrefu na kabla hajaingia kwenye eneo la hatari aliachia shuti kali lililoishia mikononi mwa kipa Hamiani.

Kipindi chote cha kwanza mechi ilionekana kupooza, kwani wageni walionekana kutaka zaidi sare, huku wakipoteza muda, hasa kipa wao ambaye mara kwa mara alikuwa akionywa na mwamuzi.

Ndipo ilipofika wakati ambao wanachama, mashabiki wa Simba na Watanzania kwa ujumla waliokuwa wakiusubiri, Sakho akafunga bao maridadi, huku wachezaji wa RS Berkane wakidhani wangeenda mapumziko wakiwa suluhu.

Kipindi cha pili Simba ilibadilika na kufanya mashambulizi mengi, na shambulio la hatari zaidi lilifanywa na Bernard Morrison sekunde chache baada ya kuingia akitokea benchi kuchukua nafasi ya Kibu Denis, aliupata mpira akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, akaachia shuti kali lililogonga kwenye maungio ya mwamba kulia mwa kipa na kurejea uwanjani.

Mbali na Kibu kutolewa, pia Simba iliwatoa mfungaji wa bao pekee Sakho, Bwalya, Kagere na nafasi zao kuchukuliwa na Mzamiru Yassin, Peter Banda, Chris Mugalu na Thadeo Lwanga.

Juhudi za wachezaji Yusuph Dayo, Ismail Mohaden, Adam Ba, Hassan El Moussadui na winga wa zamani wa Yanga, Tuisila Kisinda ziliishia miguuni mwa mabeki wa Simba, wakiongozwa na Onyango na Henoc Inonga.

Jonas Mkude nusura aipatie Simba bao la pili dakika ya 72, baada ya kumegewa pande na Shomari Kapombe, akapisha shuti kali ambalo Hamiani ambaye alifanya kazi kubwa kwenye mechi ya jana, alikwenda juu na kupangua ikawa kona.

Kwa matokeo hayo Simba imekwenda kileleni mwa Kundi D, ikiwa na pointi saba, ikicheza mechi nne, kushinda mbili, ikipoteza moja na sare moja, ikifunga mabao matano, huku ikiruhusu mabao manne kwenye wavu wake.

Kukaa kwenye nafasi ya pili kwa RS Berkane kulitegemea mechi iliyochezwa jana usiku kati ya Asec Mimosas ya Ivory Coast yenye pointi tatu, ikichezea mechi yake nyumbani nchini Benin dhidi ya US Gandamarie ya Niger iliyokuwa na alama nne. Asec Mimosas imekuwa ikichezea mechi zake za nyumbani nchini Benin.

Simba sasa inajiandaa na mechi ya ugenini dhidi ya Asec Mimosas Jumapili ijayo kabla ya Aprili 3, mwaka huu, kuhitimisha hatua hiyo ya makundi kwa kuikaribisha US Gandamarie katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >